Majukumu ya Kamati na Mratibu wa Elimu Mjumuisho

Moduli

2

Mwongozo wa Mkufunzi

SMZ
SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

MADRASA EARLY CHILDHOOD PROGRAMME

NAD – The Norwegian Association of Disabled

nfu Norsk Forbund for Utviklingshemmede

EENET Enabling Education Network

Majukumu ya Kamati na Mratibu wa Elimu Mjumuisho

Moduli ya Pili

Moduli ya Mkufunzi

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar
S.L.P 840,
Mazizini, Zanzibar info@zie.go.tz www.zie.go.tz
Simu: +255-24-2230193

Toleo la Kwanza 2022

Imetayarishwa na Enabling Education Network Machi, 2018

TEZ, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali 2022

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kwa ajili ya kuuza bila ya ruhusa ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ). Matumizi yoyote ya toleo hili kwa kunakili, kutafsiri na kukitoa kwa njia ya kielektroniki bila ya idhini ya Taasisi ya Elimu ni kosa la kisheria na utashitakiwa.

Kazi hii imepewa leseni chini ya Creative Common Attribution – Shirika lisilo la kibiashara- 4.0 Leseni ya Kimataifa. Ili kuona kivuli cha leseni, tembelea http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

Dibaji

Moduli za Elimu Mjumuisho zinalenga katika kuweka mazingira yaliyo sawa katika kuhakikisha kuwa kila mtu anashiriki ipasavyo kwenye nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika jamii ni vyema kila mmoja kutoa mchango wake katika kuijenga jamii inayohusika. Utayarishaji wa moduli za elimu mjumuisho utasaidia katika kufikia malengo yaliyowekwa katika mkutano wa Jomtien nchini Thailand (Mwaka, 1990) ambapo UNICEF ilipewa jukumu la kuhakikisha kuwa nchi zinachukua hatua za kuondokana na tafauti za elimu zinazojitokeza miongoni mwa makundi ya vijana wenye mazingira magumu. Vilevile, utayarishaji huu wa moduli za elimu mjumuisho ni matokeo ya:

- Warsha ya mafunzo ya wakufunzi iliyotayarishwa na Diakonia, Palestina, Julai 2011.
- Elimu Mjumuisho: Muongozo wa wakufunzi wa walimu, uliotayarishwa na Shirikisho la Kimataifa la Ulemavu (HIF), Cambodia, mwaka 2011.
- Programu ya mafunzo ya wakufunzi iliyoandaliwa na Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF), Macedonia, 2012–13.
- Programu ya mafunzo ya wakufunzi iliyoandaliwa na UNICEF, Libya, mwaka, 2012–2013.
- Utangulizi wa Elimu Mjumuisho: 'Mwongozo wa Wakufunzi' ulioandaliwa na HIF, Liberia, mwaka, 2012–13.

Napenda kutambua mchango wa Jumuiya za watu wenye ulemavu ya Norway (NAD) na Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa Akili, (NFU) katika kusaidia kuandika moduli za miongozo ya elimu mjumuisho na kuhakikisha kuwa zinamuongoza vyema mwalimu katika kukidhi mahitaji ya Elimu Mjumuisho. Aidha, napenda kutambua mchango wa Jumuiya ya Makuzi ya Awali ya Mtoto (MECP-Z) kwa kusimamia upitiaji wa moduli hizi. Mwisho natoa shukurani zangu za dhati kwa Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha Zanzibar kwa kuzifanyia majaribio moduli zote kwa hatua ya awali.

Ni matarajio yetu kuwa moduli za elimu mjumuisho zitatumika katika kuwaongoza walimu kukabiliana na mazingira jumuishi Zanzibar. Vile vile, wakufunzi wa vyuo vya ualimu na wahadhiri wa vyuo vikuu watatumia miongozo hii kwa ajili ya kuhakikisha walimu wanapata uzoefu katika kukabiliana na mazingira ya elimu mjumuisho; Zanzibar.

____

Khamis Abdulla Said
Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar.

Shukurani

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) inatoa shukurani zake za dhati kwa taasisi mbali mbali zilizohusika katika kutayarisha na kupitia moduli hizi za elimu mjumuisho. Taasisi hizo ni pamoja na; Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha Zanzibar, Idara ya Mafunzo ya Uwalimu, Vyuo vya Uwalimu na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Aidha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Jumuiya ya Makuzi ya awali ya mtoto (MECP-Z) zimehakikisha kuwa moduli zilizotayarishwa zinamuongoza vyema mwalimu katika kukidhi mahitaji ya mazingira ya Elimu Mjumuisho.

Aidha, Wizara inawashukuru wale wote waliotayarisha moduli na zana zote na kuzifanyia majaribio kwa ushirikiano na wafanyakazi wa Mtandao wa Kuwezesha Elimu (EENET) na washauri kutoka maeneo mbalimbali barani Afrika, Asia na Ulaya kwa kipindi cha miaka 10 au zaidi.

Mwisho natoa shukurani zangu za dhati kwa Wafadhili wa Elimu Zanzibar kupitia Jumuiya ya watu wenye ulemavu ya Norway (NAD) kwa kuendelea kushirikiana na WEMA katika kufanikisha uandaaji wa mwongozo huu.

____

Abdalla M. Mussa
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Elimu ya Zanzibar

Yaliyomo

Vifupisho....8

Utangulizi....9

Kipindi cha 2.1: Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli....11

Kipindi cha 2.2: Ni kwa Namna gani Kamati ya Elimu Mjumuisho husaidia Skuli kuwa Jumuishi zaidi?....20

Kipindi cha 2.3: Uundaji wa Kamati ya Elimu Mjumuisho....24

Kipindi cha 2.4: Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli....31

Kipindi cha 2.5: Sifa za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli....35

Kipindi cha 2.6: Jukumu la Mtaratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli hati ndogo ziwe kubwa....40

Kipindi cha 2.7: Mtazamo wa Skuli kwa Elimu Mjumuisho ni Jukumu la Msingi la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli....49

Kipindi cha 2.8: Kuanzisha na Kuvibadilisha Vituo Saidizi vya Ujifunzaji ili kupelekea Ufanisi katika Ujumuishi....54

Kielelezo nambari 2.1: Kisa Mafunzo cha Kamati ya Skuli ya Mjumuisho....59

Kielelezo nambari 2.2: Mbinu pacha....63

Kielelezo nambari 2.3: Ufupisho wa Kamati ya Elimu Mjumuisho....64

Kielelezo nambari 2.4: Kisa Mafunzo – Maana ya Kamati ya Skuli ya Mjumuisho?....65

Kielelezo nambari 2.5: Uhusiano wa Madaraka.....68

Kielelezo nambari 2.6: Walimu Wakuu wanatafakari juu ya Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli....70

Kielelezo nambari 2.7: Kuandikisha Wajumbe wa Kamati.....72

Kielelezo nambari 2.8: Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli anafanya nini? 74

Kielelezo nambari 2.9: Taarifa za Majadiliano....75

Kielelezo nambari 2.10: Sifa za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli....76

Kielelezo nambari 2.11: Maonesho ya Igizo-dhima....77

Kielelezo nambari 2.12: Muonekano wa Mtazamo wa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli 79
Kielelezo nambari 2.13: Mifano ya Vitendo ambavyo Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli anaweza Kushiriki 80
Kielelezo nambari 2.14: Hadithi ya Jabir 82
Kielelezo nambari 2.15: Kufanya kazi kuelekea Mjumuisho 83
Kielelezo nambari 2.16: Wanafunzi, Wazazi na Walezi wanasema nini? 86
Kielelezo nambari 2.17: Igizo dhima la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli 88
Kielelezo nambari 2.18: Matumizi Bora ya Vituo Saidizi vya Ujifunzaji 93

Rejea 94

Vifupisho

EENET	Enabling Education Network
MECP-Z	Madrasa Early Childhood Program-Zanzibar
NAD	Norwegian Association of Disabled
NFU	Norsk Forbund for Utviklingshemmede [Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa Akili Norway]
TEZ	Taasisi ya Elimu ya Zanzibar
UNICEF	United Nations International Children’s Emergency Fund
WEMA	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Utangulizi

Lengo la Moduli hii ni kuwasaidia walimu na wadau wengine, kama vile wafanyakazi wa skuli wasiokuwa walimu, wafanyakazi wa elimu katika ngazi ya wilaya, jamii na watu wengineo katika kupanga, kusimamia na kuziendeleza kamati za elimu mjumuisho za skuli. Hii inajumuisha kuwajengea uwezo wa kujiamini, kuwajibika, kupata ujuzi na maarifa, na kuwawezesha kinadharia na kivitendo.

Moduli hii inakuza uwezo wa walimu kujitafakari, kutoa ushauri na kujengeana uwezo miongoni mwao katika utekelezaji wa Elimu Mjumuisho na kuwa mfano katika mambo yote yanayohusiana na Elimu Mjumuisho ndani ya skuli. Kama ilivyo katika moduli ya kwanza, "Utangulizi wa Elimu Mjumuisho." Pia, moduli hii inazingatia mtazamo mahsusi wa kuwajumuisha wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji ya ziada, kama vile mahitaji maalumu ya kielimu au watu wenye ulemavu, ambao mara nyingi wanakosa fursa na wanatengwa. Inashauriwa kuwepo kwa uhamasishaji wa elimu mjumuisho katika ngazi ya skuli na jamii sambamba na kuwapatia ushauri na mafunzo, ili kuwawezesha kubadilishana uzoefu katika ngazi ya skuli na jamii.

Pia, moduli hii inaelezea dhana ya wasimamizi wa Elimu Mjumuisho, katika muundo wa waratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli na wengineo ambao wanafanya kazi kwa karibu na Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli.

Vitendo katika moduli hii inajumuisha kuandaa na kuimarisha uhusiano baina ya skuli, wanafunzi, wazazi au walezi, jamii pamoja na wataalamu wengine.

Miongoni mwa majukumu ya mratibu wa Elimu Mjumuisho ni kuanzisha na kushajiisha ushirikiano kwa ajili ya ujumuishaji. Moduli hii itatoa fursa ya majadiliano na kubadilishana mawazo juu ya mada hii.

Taarifa za ziada zinapatikana katika moduli ya ziada ya "Ushirikishwaji wa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada". Moduli hii ya ziada ina manufaa sana, hasa ukizingatia changamoto zinazowakabili waratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli na inaweza kutumika kama msingi wa rejea katika moduli yote.

Wakufunzi wanapaswa kuzingatia kwamba, moduli hii inalenga katika kutoa ushauri kwa walimu na wadau wengine kuhusu kamati za Elimu Mjumuisho za skuli na kuwapa njia tafauti ambazo wangeweza kuzitumia katika kuziunda na kuziendesha. Sambamba na hilo, ingawa Moduli hii inapendekeza njia

mbalimbali ambazo washiriki wanaweza kuzitumia. Pia, wako huru kutumia mbinu nyengine zinazohusika ambazo hazikutajwa katika Moduli hii. Hii ni kwa sababu kila skuli inahitaji kamati na waratibu wa elimu mjumuisho wa skuli ambao wanaweza kubadilika na kuendana na mazingira yaliyopo, kuweza kutatua matatizo yaliyowazunguka na kutumia fursa zilizopo. Hii inamaanisha kwamba, hakuna kanuni maalumu ambazo washiriki wanaweza kufunzwa. Kwa mnasaba huo, hakuna njia mahsusi ambayo watalazimika kuifuata katika kutoa taarifa za msingi na mifano halisi, Moduli hii itawarahisishia walimu, wanataaluma na wadau wengine kuendeleza fikra ambazo zitasaidia kuimarisha skuli zao. Pia, zitawawezesha kuanza kufanya kazi kwa pamoja kama Kamati ya Elimu Mjumuisho ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Mwisho, Moduli hii inajadili uwezekano wa kuvianzisha na kuviendeleza, “Vituo Wezeshi vya Ujifunzaji” katika kuratibu elimu mjumuisho na vipindi vyote vya mafunzo na kuzisaidia kazi za vitendo vya wanafunzi wenye mahitaji ya ziada.

Suala la kujadili ni hili: “ni majukumu yepi ambayo Mratibu wa elimu mjumuisho katika skuli anapaswa kuyazingatia katika kuanzisha na kuendeleza matumizi sahihi ya Vituo Wezeshi vya Ujifunzaji”.

Muda wa Mafunzo

Mkufunzi anapaswa kurekebisha mafunzo haya ili kwenda sambamba na mazingira halisi na muda utakaowekwa kwa ajili ya mafunzo. Mkufunzi anaweza kuamua kutotumia kazi zote za vitendo, au kupunguza baadhi ya kazi za vitendo, iwapo muda hautoshi au kuongeza kazi za vitendo kama washiriki watahitaji kufahamu zaidi mada inayohusika.

Iwapo kazi zote za vitendo zitatumika, bila ya marekebisho ya msingi (kufupisha au kurefusha) Moduli hii itahitaji kiasi cha saa 14 za mafunzo. Saa hizi zitagaiwa kwa siku mbili hadi tatu, kutegemea na ratiba ya mafunzo kwa siku.

Kipindi cha 2.1: Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli

Utangulizi

Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli inajumuisha watu wenye mwamko wa elimu katika skuli zao na ambao wana lengo moja katika kuifanya skuli yao kuwa ya mjumuisho.

Vipindi vya 2.1, 2.2 na 2.3 vinawasaidia walimu, wanataaluma wengine, wanajamii na wadau mbali mbali kupanga, kusimamia na kuziendeleza kamati za Elimu Mjumuisho za skuli. Hii inajumuisha kuwajengea uwezo wa kujiamini, ujuzi, uwajibikaji na maarifa, pamoja na kuwawezesha kujifunza kinadharia na vitendo.

Kila skuli inahitaji Kamati ya Elimu Mjumuisho ambayo inaweza kubadilika na kwenda sambamba na mazingira yaliyopo, kuweza kutatua matatizo yaliyowazunguka na kutumia fursa zilizopo. Kulingana na hilo, walimu, wafanyakazi wasiokuwa walimu na wadau wengine katika jamii watahitajika kuendeleza fikra zitakazoimarisha skuli zao. Hakuna kanuni maalumu ambazo washiriki wanaweza kufunzwa. Ni sawa kusema kwamba, hakuna njia mahsusi ambazo watalazimika kuzifuata. Kwa kutoa taarifa za msingi na mifano halisi, vipindi hivi vitawarahisishia walimu, kuendeleza fikra ambazo zitasaidia kuimarisha skuli zao. Pia, vitawawezesha kuanza kufanya kazi kwa pamoja ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Kitendo cha 2.1a: Nini Maana ya Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli?

Kikuu

Muda: Dakika 30

Mkufunzi anapaswa kutumia kitendo hiki ili afahamu mawazo waliyonayo washiriki kuhusu:

- Maana ya Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli na inafanya kazi gani?

Kwa kufanya kazi mmoja mmoja, washiriki watatakiwa kuchora mchoro juu ya wanachofikiria kuhusu maana ya Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli na kazi zake inazopaswa kuzifanya. Mkufunzi anapaswa kuwahakikishia washiriki kuwa, kitendo hiki si mtihani bali ni namna tu ya kupata mawazo yao.

Kila mshiriki atakaa na mwenzake aliyekaribu naye, kisha watabadilishana kazi zao na kuchangiana mawazo. Kisha kila jozi itapaswa kukamilisha sentensi hii:

- "Tunafikiri Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli ni...   "

Mkufunzi anatakiwa aongoze mrejesho uliokamilika na aandike nukta muhimu katika chati. Iwapo mshiriki mmoja wapo atawasilisha mawazo ambayo hayapo katika jukumu la Kamati ya Elimu Mjumuisho, mkufunzi anatakiwa awasilishe hili kiusahihi na awatake washiriki kutafakari ni kwanini Kamati ya Elimu Mjumuisho haikuwa sahihi kulifanya hili. Mfano: Kamati ya Elimu Mjumuisho haina mamlaka ya kumpa adhabu au kumfukuza kazi mwalimu ambaye anakwenda kinyume na taratibu za elimu mjumuisho.

Mfano wa ramani ya kumbukumbu ya muundo wa Kamati ya Elimu Mjumuisho



[Maelezo ya picha: Mchoro wa duara katikati ambao umeandikwa 'Kamati ya Elimu Mjumuisho'. Maduara mengine 8 yamezunguka duara la kati, lililounganishwa katikati na mistari. Maduara yaliyo karibu yana maneno kama vile 'walimu, wazazi na jamii.]

Kitendo cha 2.1b: Uchambuzi wa Kisa Mafunzo

Kikuu

Muda: Dakika 60

Kitendo hiki kitawawezesha washiriki kuwa na uzoefu na mfano halisi wa Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli. Kamati ya elimu mjumuisho itawasaidia kuifanyia zoezi mbinu ya ramani ya kumbukumbu ambayo itapelekea kushirikiana katika kufikiri na kuchambua mambo mbalimbali yatakayoimarisha Elimu Mjumuisho.

Kielelezo nambari 2.1

Kisa Mafunzo juu ya Kamati ya Elimu Mjumuisho

Katika vikundi vyao, Mkufunzi awatake washiriki wasome kisa mafunzo kutoka **Kielelezo nambari 2.1** na kujadili swali moja

Mkufunzi anapaswa kukipa kila kikundi swali moja, ambapo kila swali litajadiliwa na kikundi kimoja. Maswali yenyewe ni;

- Kamati ya Elimu Mjumuisho inafanya kazi gani?
- Ni nani anayehitajika kuhusishwa katika kamati? Wanahusishwa kwa namna gani?
- Ni changamoto gani zinazowakabili katika utekelezaji wa kazi za kamati?
- Wamefanya nini katika kutatua changamoto hizo?
- Je, ni mapendekezo gani ungewapa ili kuboresha na kukuza kazi zao?

Baada ya kuandika orodha ya majibu, kila kikundi kitalazimika kuweka kumbukumbu ya mawazo yao katika mfumo wa **ramani ya kumbukumbu** – mchoro unaweza kuwa na neno moja au kifungu cha maneno katikati, na baadae mawazo, maneno au dhana zinazohusiana na neno au kifungu hicho cha maneno zitaandikwa pembeni yake. Ramani ya kumbukumbu inaweza kuwiana **na** uteuzi kwa mbinu ya kujifunza kwa kuona, ambapo pia ukaoana na wanaopenda kujifunza kupitia majadiliano au kwa kuandika maneno.

Ramani ya kumbukumbu inakuwezesha kuona muunganiko na uhusiano baina ya maswala tafauti, watu na matukio . Rangi tafauti, maumbo na mishale inaweza kutumika kutafautisha aina mbalimbali za taarifa na uhusiano.

Mfano; maandishi mekundu yanaweza kuonesha mawazo hasi wakati maandishi ya kijani yanaweza kuonesha mawazo chanya.

Mkufunzi anaweza kuhitaji kuwaonesha washiriki mfano wa ramani ya kumbukumbu ikiwa hawakuwahi kuitumia mbinu hii kabla. Sampuli zinaoneshwa hapo chini, lakini pia mkufunzi anaweza kutumia mifano katika warsha zilizopita ambazo walizowahi kuzifanya. Mkufunzi anapaswa kusisitiza kuwa hakuna njia sahihi au isio sahihi ya kufanya ramani ya kumbukumbu, hivyo ni sawa kwa kila kikundi kubuni michoro tafauti.

Washiriki wakitengeneza ramani ya kumbukumbu

[Maelezo ya picha: Mchoro wa hapo juu unaonesha wanaume wawili na wanawake watatu wakiwa wamezunguka meza, mwanamme mmoja anaandika kwenye karatasi iliyopo katikati ya meza.]



Mchoro Na. 1: Mfano wa mchoro wa ramani ya kumbukumbu

[Maelezo ya picha: Ramani ya kumbukumbu, iliyo na duara lisilo na maandishi, halafu visanduku na viduara vyengine tafauti vimeunganishwa kwa mistari na mishale.]

Mchoro Na. 2: Mfano wa ramani ya kumbukumbu iliyobuniwa na walimu waliofikiria namna ambavyo skuli inaweza kuwa jumuishi.

Mkufunzi atumie moja kati ya mbinu za mrejesho zifuatazo ili kuwezesha mrejesho uliokamilika, majadiliano ya pamoja na kufafanua nukta zenye utata ambazo zimejitokeza. Nukta hizo zinapaswa kuandikwa katika chati kwa ajili ya kuweka kumbukumbu. Mkufunzi anapaswa:-

- Kuangalia kila swali kwa zamu kisha awatake walijadili swali hilo kubainisha nukta muhimu.
- Awatake kila kundi kuwasilisha na kuelezea nukta muhimu kwa mujibu wa maswali waliyojadili.
- Awatake kila kundi kuweka ukutani kazi zao, kisha washiriki wote wazipitie kazi zote na kuwataka kundi ambalo kazi yake ipo ukutani kuelezea nukta muhimu walizoziandika.

Wakati wa majadiliano, mkufunzi anaweza kufanya rejea kutoka katika ramani za kumbumbu za washiriki wa warsha zilizopita



Ramani ya kumbukumbu iliyotayarishwa na washiriki.

[Maelezo ya picha: Ramani ya kumbukumbu, ina duara katikati lenye neno Kamati ya Elimu Mjumuisho. Kuna maduara matatu yamebeba maneno yanayotoa mawazo “Kamati ya Elimu Mjumuisho inafanya nini” maduara hayo yanaeleza “changamoto” “suluhisho”. Kila duara limeunganishwa na duara la kati kwa kutumia mshale.]

Kitendo cha 2.1c: Mbinu Pacha

Kikuu

Muda: Dakika 10

Elimu mjumuisho inalenga kubadilisha mfumo na sio kumbadilisha mwanafunzi. Hata hivyo, kwa kuzingatia mabadiliko ya kiwango cha mfumo, haimaanishi kwamba tunapaswa kupuuza mahitaji mahsusi ya kila mwanafunzi. Tunahitaji kukabiliana na mitazamo ya kutotiliwa maanani kwa Elimu Mjumuisho katika namna mbili: Namna hizo ni kuimarisha mabadiliko ya kimfumo na kwa kutoa msaada maalumu kulingana na mahitaji ya kujifunza kwa kila mwanafunzi. Hii ndio inaitwa mbinu pacha.



Mchoro Na. 3: Mbinu pacha

Mkufunzi awape washiriki **kielelezo nambariri 2.2** na kuwakumbusha washiriki daima wanapaswa kuzingatia njia zote mbili za ujumuishi- kubadilisha mfumo na jamii ili kuwa mjumuisho zaidi. Pia, kutoa msaada unaofaa kwa wanafunzi mahsusi pale inapohitajika. Hii ni mbinu-pacha ya ujumuishi.

Kielelezo nambari 2.2 **Mbinu Pacha**

Kitendo cha 2.1d: Marudio Maana ya Kamati ya Elimu Mjumuisho

Kikuu

Muda: Dakika 20

Mkufunzi awatake washiriki kutazama tena michoro waliyochora (**Kitendo cha 2.1a**) na chati yenye nukta muhimu zilizoibuliwa kwa michoro na **kitendo cha 2.1b**. Kisha mkufunzi awaulize:

- Je kila mmoja bado anafikiria kuwa orodha hii inaakisi maana halisi ya Kamati ya Elimu Mjumuisho na kazi zake?
- Je orodha inaonesha uwelewa wa mbinu pacha, ambayo imelenga kufikia mahitaji ya mwanafunzi mmoja mmoja pamoja na mabadiliko ya mfumo? Je unaweza kutoa mfano?
- Kuna yeyote anayeweza kuongeza au kusahihisha chochote? Kwa nini?

Pia, mkufunzi anaweza kuwasilisha na kuelezea Kamati ya Elimu Mjumuisho.

Tazama **Kielelezo nambariri 2.3**. Pia, watake washiriki kutafakari juu ya kitu chochote ambacho hawakukifikiria hapo awali.

Kielelezo nambariri 2.3

Muhtasari wa Maana ya Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli

Iwapo washiriki bado hawakufahamu maana ya Kamati ya Elimu Mjumuisho, mkufunzi watake washiriki kufanya mazoezi katika vikundi vyao kwa kutumia **Kielelezo cha 2.4** kwa kusoma visa mafunzo ili kuweza kueleza maana ya Kamati ya Elimu Mjumuisho - kumbuka kwamba hakuna jibu sahihi au lisilosahihi kabisa.

Kielelezo nambari a 2.4

Visa Mafunzo: Nini Maana ya Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli?

Kipindi cha 2.2: Ni kwa Namna gani Kamati ya Elimu Mjumuisho husaidia Skuli kuwa Jumuishi zaidi?

Utangulizi

Katika kipindi hiki washiriki watafikiria namna ya kujenga mawazo ya kwa namna gani Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli inaweza kuwa na uhalisia kwa mujibu wa mazingira yao. Kwa kufahamu ni vipi ingeweza kuwasaidia, pia wahamasishwe namna ya kutumia muda na nguvu katika kuunda kamati hiyo ili ipate mafanikio.

Kitendo cha 2.2a: Matatizo Gani ambayo Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli husaidia Kuyatatua?

Kikuu

Muda: Dakika 30

Washiriki watapaswa kufanya kazi katika vikundi vidogo vidogo, hususan wale waliotoka katika skuli moja, kujadili swali lifuatalo:

- Eleza changamoto unazokumbana nazo katika skuli yako pamoja na kwamba wanafunzi wanahudhuria skuli vizuri, wanashiriki katika mchakato wa kujifunza, na kuyafikia malengo ya kujifunza kadiri ya uwezo wao.

Mkufunzi anatakiwa kuwahamasisha washiriki kufikiria na kuzingatia kwa kina kuhusu kiwango kikubwa cha wanafunzi walio katika hatari ya kutengwa. Kwa mfano, wanafunzi wenye mahitaji ya ziada, kama vile: mahitaji maalumu ya kielimu au wenye ulemavu, wakiwemo; wanaozungumza lugha tafauti, wale waliotoka katika familia masikini sana, wenye matatizo ya kitabia na mihemko, waliotoka katika jamii za watoto ambazo hazina watu wengi wa kike na wa kiume , wenye matatizo ya kiafya, waliopoteza mzazi mmoja au wote wawili na kukumbuka modeli ya mtazamo wa kijamii ambayo ilijadiliwa hapo kabla, kwamba tatizo haliko kwa mwanafunzi mwenyewe bali liko kwa jamii na kwenye mfumo wa elimu.

Kila kikundi cha washiriki kinapaswa kuandika changamoto walizozigundua katika vipande vya karatasi na kubandika ukutani kwa muundo wa tofali. Kila kipande cha karatasi chenye muundo wa tofali kioneshe changamoto ambazo zinamzuia mwanafunzi kupata fursa ya kwenda skuli, kushiriki na kupata

mafanikio. Washiriki wahamasishwe kufanya vitu vinavyofanana watakaporejea katika skuli zao, sambamba na kufanya uchambuzi wa vikwazo wakishirikiana na marafiki zao, wazazi/walezi na watoto wote.



Mchoro Na. 4: Mfano wa mchoro wa ukuta wa matofali

[Maelezo ya picha: Mchoro huu unaonesha sehemu ya ukuta uliotengenezwa kwa matabaka 7 ya matofali. Matofali mengine yana maneno yaliyoandikwa juu yao kuelezea aina ya vikwazo au changamoto.]

Mfano wa mchoro wa ukuta wa matofali.

[Maelezo ya picha: Vipande vya karatasi vimebandikwa ukutani. Kila kipande cha karatasi kinaonesha kikwazo kilichoandikwa juu yake. Kwa mfano; “hakuna mafunzo ya kutosha kwa walimu", na 'mtazamo hasi'. Mwanamme amesimama upande wa kulia wa picha hiyo, akibandika karatasi hizo ukutani.]

Kitendo cha 2.2b: Ni kwa namna gani Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli inavyoweza Kusaidia Kutatua Vikwazo vya ujumuishaji?

Kikuu

Muda: Dakika 30-45

Katika kitendo hiki washiriki watatafakari zaidi, hususan katika vikwazo vya ujumuishaji na michango inayohitajika katika kutatua vikwazo hivyo, vile vile kutafakari njia ambazo zitakazowezesha Kamati za Elimu Mjumuisho za skuli kuwa bora zaidi.

Katika vikundi vidogovidogo, washiriki wachague vipande vya matofali (vikwazo) vichache kutoka katika ukuta na kuvijadili kama ifuatavyo;

- Ni kwa namna gani kikwazo hiki kitatatuliwa? Ni hatua zipi za kivitendo zitachukuliwa?
- Nani anapaswa kushirikishwa katika kuchagua, kuendeleza na kutekeleza suluhisho linalohitajika kutatua vikwazo husika? Je kila mmoja atafanya nini?
- Ni kwa namna gani kufanya kazi kwa pamoja kutapelekea ufanisi zaidi katika kutatua kikwazo hiki kuliko kama mtu mmoja angetatua peke yake.

Washiriki waandike majibu yao katika jaduweli lifuatalo:

Kikwazo	**Ni kwa namna gani kikwazo hiki kitatatuliwa?**	**Nani anayepaswa kushirikishwa? Je Kila mmoja atafanya nini?**	**Ni kwa namna gani kufanya kazi kwa pamoja kutapelekea ufanisi zaidi katika katatua kikwazo hiki kuliko kama mtu mmoja angetatua peke yake.**
(Elezea kikwazo cha kwanza (1)			
[Elezea kikwazo cha pili (2)			
[Elezea kikwazo cha tatu (3)			

Jaduweli Na. 1: Vikwazo

Washiriki watakiwe kufikiria juu ya mfanano wa majibu yao katika kila kikwazo. Mfano, suluhisho ambalo lingeweza kutatua kikwazo zaidi ya kimoja. Baadae, mkufunzi atawaongoza washiriki kutoa mrejesho sahihi.

Mfano wa uchambuzi wa jaduweli la vikwazo

[Maelezo ya picha: Karatasi kubwa iliyobandikwa ukutani, imegawanywa katika vipengele vinne 4 navyo ni 'vikwazo', ' namna gani?', 'nani?', 'nini?'. Majibu yameandikwa chini ya kila kipengele.]

Kipindi cha 2.3: Uundaji wa Kamati ya Elimu Mjumuisho

Utangulizi

Uundaji wa Kamati ya Elimu Mjumuisho unaweza kuwa si jambo rahisi isipokuwa kila mjumbe aonekane kuwa ni sawa na wengine katika kamati na kwamba wajumbe wote wanaweza kuwa na michango tafauti mawazo na uzoefu walionao ambao utasaidia katika kufanikisha elimu mjumuisho.

Kitendo cha 2.3a: Mahusiano ya Kimadaraka

Kikuu

Muda: Dakika 30

Mchezo huu unawasaidia washiriki kufikiria kuhusu umuhimu wa uhusiano wa usawa katika Kamati ya Elimu Mjumuisho. Kamati inaweza kuwa na mratibu lakini mtu huyu asiwe na madaraka zaidi kuliko mjumbe mwengine katika kamati. Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli haitaweza kufanikiwa iwapo itatumika kama nyenzo ya kuongeza madaraka ya mtu binafsi.

Mkufunzi aweke alama mbili, katika pembe tafauti za chumba: moja iwe inasema 'ana madaraka zaidi' na nyengine 'hana madaraka.' Inapaswa kuwepo na nafasi iliyo wazi baina ya alama zote mbili. Kisha, mkufunzi ampe kila mshiriki kitambulisho ambacho kitaelezea kazi au cheo. Angalia mfano katika sanduku la chini.

Mkufunzi awatake washiriki wote wajifanye kuwa wanaume. Washiriki wajipange katika 'mstari wa madaraka' inategemea ni kwa jinsi gani watafikiria mwanamme mwenye kazi hiyo kuwa ni mwenye madaraka au hana madaraka. Hali hii waihusishe zaidi na uhalisia wa jamii zao na sio kama hali ilivyojitokeza.

Washiriki wanaweza kujadiliana na kuhamasishana kwa kila mmoja kwa kubadilisha nafasi.

Washiriki wakiwa katika kitendo cha mahusiano ya madaraka

[Maelezo ya picha: Takribani washiriki 12 wanaume na wanawake wamesimama kwa mstari kila mmoja akiwa amevaa kitambulisho.]

Mawazo kuhusu stika za kazi au cheo

- Mwalimu wa darasa la kwanza mwenye uzoefu wa miaka mitatu
- Mtaalamu wa matamshi
- Mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo mwenye umri wa miaka 6
- Mtaalamu wa tiba ya viungo
- Hakimu
- Mwanasaikolojia
- Muuguzi wa skuli
- Mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili mwenye umri wa miaka 9
- Mtabibu
- Mwanafunzi asiyekuwa na ulemavu mwenye miaka 7
- Afisa wa polisi
- Mtu mzima mwenye ulemavu anayeishi karibu na skuli
- Kiongozi wa kijiji
- Mpishi wa skuli
- Ndugu wa mwanafunzi mwenye ulemavu

- Msaidizi wa darasa
- Mhadhiri wa chuo kikuu
- Mwalimu wa darasa la 5 mwenye uzoefu wa miaka 25
- Mzazi au mlezi wa mwanafunzi mwenye mahitaji ya ziada
- Mwalimu mkuu
- Mlezi wa skuli
- Mwalimu wa michezo
- Dereva wa basi
- Mkulima
- Mwalimu wa kidato cha pili mwenye uzoefu wa mwaka mmoja
- Liwali wa skuli
- Mzazi, mlezi au muangalizi asiyeajiriwa wa mwanafunzi asiye mlemavu
- Mtunza usafi
- Mzazi,mlezi au muangalizi ambaye ni mjumbe wa kamati ya wazazi na walimu

Jaduweli Na. 2: Mawazo kuhusu stika za kazi au cheo

Mkufunzi anaweza kubadilisha nafasi hizi ili kulingana na muktadha wa mafunzo

Baadhi ya washiriki watapewa stika ambayo inaelekeza kujifanya kuwa ni wanawake. Ni lazima waamue na wajadiliane ama wakae juu ya mstari au nje ya mstari, inategemea ni vipi wanafikiria juu ya ipi hadhi ya mwanamke inayomfanya kuwa au kutokuwa na 'nguvu au madaraka' katika jamii anayoishi.

Mwisho, kama muda upo, mkufunzi aondoe stika kwa baadhi ya washiriki, stika zitakazoondolewa ni zile zinayozungumzia juu ya ulemavu, hali ya afya au hali ya kiuchumi. Mfano kutokuona, ulemavu wa viungo, masikini sana, wenye matatizo ya matamshi, wakimbizi, wazee, wenye virusi vya UKIMWI n.k. Washiriki kwa mara nyengine tena watathmini na wajadiliane iwapo nafasi zao katika mstari zinahitaji kubadilishwa.

Majadiliano mafupi ya pamoja kuhusu masuala ya madaraka yatafuata. Kujadili kwanini baadhi ya watu wanakuwa wana nguvu zaidi kuliko wengine na vipi

inaweza kuathiri juhudi za kuifanya elimu kuwa jumuishi zaidi?

Kielelezo nambariri 2.5 **Uhusiano wa Madaraka**

Mkufunzi awasilishe baadhi au taarifa zote kutoka katika **kielelezo nambari 2.5**

Kitendo cha 2.3b: Uandikishaji wa Wajumbe wa Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli

Kikuu

Muda: Dakika 45

Kabla ya kuzingatia utaratibu wa usajili wa wajumbe wa Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli, mkufunzi aoneshe vidio fupi yenye walimu wakuu watatu wanaoelezea muundo na majukumu ya wajumbe wa kamati hiyo.

Kielelezo nambariri 2.6 **Walimu Wakuu Kutafakari juu ya Kamati zao za Elimu Mjumuisho**

Mkufunzi atampatia kila mshiriki nakala ya kielelezo nambari 2.6 awaeleze kuwa nakala hizo zimo katika video ambayo wanatarajia kuiangalia.

Aoneshe video ambayo itatumia muda wa dakika 3 na sekunde 34. Awatake washiriki waandike mambo yote yatakayojitokeza kwenye filamu na ambayo wangependa kuyajadili. Mwisho wa filamu awatake washiriki kubadilishana mawazo na kujadili mambo yote ambayo wangependa kuyazingatia.

Baada ya mjadala mfupi, mkufunzi asisitize maneno ya mwalimu mkuu mmoja ambaye alieleza katika filamu kwamba, “Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli, ni muhimu sana kwetu, kwa sababu, tumeweza kuwa karibu zaidi na watoto kuliko ziara tunazozifanya majumbani mwetu”.

Mkufunzi aelezee umuhimu wa maneno ya mwalimu mkuu, kwa hivyo, watu wanaostahiki ndio wanaopaswa kusajiliwa kujiunga na Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli. Awatake washiriki kufikiria ni kwa namna gani wanaweza kuwavutia watu wenye maarifa, elimu, utayari na uzoefu kwenye Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli kwa utaratibu wa kujitolea.

Jambo hili haliwezi kuwa rahisi hasa ukizingatia kwamba Elimu Mjumuisho ni dhana mpya katika skuli, walimu wanaweza kuhisi kuwa wametwishwa mzigo mkubwa. Mazoezi haya yatawasaidia washiriki kufikiria ni kitu gani kitawavutia wengine kujiunga na kamati na kwa namna gani watafanikiwa kuandikisha wajumbe wa kamati. Jambo muhimu ni kwamba kamati inapaswa kuwa na wajumbe ambao wako tayari kufanya kazi kwa kujitolea na si kwa kulazimishwa.

Mkufunzi awaweke kila kundi la washiriki katika kundi lengwa ambalo linaweza kuwavutia kujiunga na Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli, kwa mfano:

- Mwalimu wa kawaida
- Mwalimu mkuu au Msaidizi mwalimu mkuu
- Wataalamu wengine
- Mzazi au mlezi au msimamizi wa watoto
- Wanafunzi wanne ambao wanajiamini na wanaweza kujielezea, (wasichaguliwe kwa sababu ya kuwa na alama za juu za masomo).
- Mtaalamu au wataalamu wa nje – washiriki wanaweza kuandika katika kadi kubainisha utaalamu maalumu ikiwa watataka kufanya hivyo, mfano mwanasaikolojia, mfanyakazi wa kijamii, wakaguzi kutoka ofisi ya mkaguzi mkuu wa elimu nk
- Wafanyakazi wasiokuwa walimu katika skuli. Kwa mfano mpishi na mlezi.
- Wanajamii
- Wajumbe wa jumuiya ya kijamii kwa mfano: jumuiya ya watu wenye ulemavu (DPO).

Washiriki katika kikundi cha kwanza wawahamasishe wawakilishi wa walimu kujiunga na kamati, washiriki katika kikundi cha pili wawahamasishe wawakilishi wa wanafunzi kujiunga na kamati na washiriki katika kikundi cha tatu wawahamasishe wazazi au walezi wa watoto kujiunga katika kamati n.k. Idadi ya washiriki na muda ndivyo vitakavyojulisha kama vikundi lengwa vyengine vimeachwa.

Katika vikundi vyao, washiriki wanapaswa kufikiria yafuatayo:

- Kitu gani kitamvutia mtu kutoka katika kundi la watu ili kujitolea kuwa mjumbe wa Kamati ya Elimu Mjumuisho? Fikiria kuhusu ushawishi wa mtu binafsi na unaotokana na taaluma au kazi ya mtu. Mbinu gani zitumike kwa ajili ya kufikisha taarifa zinazohusu kuwepo kwa Kamati ya skuli ya Elimu

Mjumuisho na kazi za kamati hiyo?

- Ni ujumbe gani ungetumika kuvishawishi vikundi vya watu kujiunga na Kamati ya Elimu Mjumuisho?

Iwapo muda unaruhusu, baada ya kujibu maswali hayo washiriki waweze kubuni au kutayarisha vifaa ambavyo wangeweza kuvitumia kwa kulielezea kundi lengwa kuhusu Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli na kuwashawishi watu kujiunga. Jambo hilo linaweza kujumuisha vipeperushi, barua, kuandaa mkutano au mchezo wa kuigiza n.k.

Mara baada ya kumaliza wanaweza kubadilishana mawazo juu ya walichokipanga. Katika vikundi vyao. Vikundi vyengine vinapaswa kutoa mawazo yenye kujenga na kupendekeza kwa ajili ya kuimarisha kamati.

Kielelezo nambariri 2.7 **Kuwaandikisha Wajumbe wa Kamati**

Mkufunzi anapaswa kuchukua maelezo yanayotokana na kikao cha jumla na pia anaweza kuchagua kujaza mapengo kwa kuwasilisha hoja kuu kutoka **Kielelezo nambari 2.5**.

Kitendo cha 2.3c: Uundaji wa Kamati

Kikuu

Muda: Dakika 30

Maelekezo kwa Mkufunzi
Katika kitendo hiki mkufunzi awashawishi washiriki kutafakari jinsi ya kuiwezesha Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli kufanya kazi kwa pamoja na kwa ufanisi. Kamati bora ya Elimu Mjumuisho inahitaji wajumbe wa aina tafauti ili kuwasilisha maoni na uzoefu wao, lakini watu ambao wanatoka katika mazingira tafauti hawawezi kufanya kazi pamoja kwa misingi ya usawa. Mratibu wa kamati atakua na jukumu la kuiunda kamati na hivyo kitendo hicho kitawawezesha washiriki kujadiliana kuhusu wazo hilo.

Pia, kufanya kazi katika vikundi, washiriki wabuni zoezi litakalounda kamati ambayo itashirikiana kufanya kazi na mratibu wa kamati pamoja na wajumbe wengine. Hali hii itapelekea kujuwana na kufanya kazi kwa furaha. Kupitia vitendo mbalimbali vilivyofanyika wakati wa mafunzo, mkufunzi awakumbushe

washiriki kuwa tayari kutumia vitu mbalimbali walivyojifunza kupitia warsha hiyo. Kama kutakuwa na muda vikundi vitatakiwa kuonyesha kazi zao kwa washiriki kutoka katika vikundi vyengine.

Washiriki wakifanya kazi katika kuunda kamati

[Maelezo ya picha: Wanawake watatu na wanaume wawili wamezunguka meza. Mwanamke mmoja anazungumza huku ameinua mkono na wengine wanaangalia, wanasikiliza na baadhi yao wanaandika.]

Kipindi cha 2.4: Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli

Utangulizi

Walimu wengi na wanataaluma wengine wanafanya kazi katika mazingira magumu. Hata hivyo, wanajitahidi ili kuyafikia mahitaji ya wanafunzi wanaowafundisha. Wanajitolea kwa kiwango cha hali ya juu kwenye kazi zao lakini wanakosa mambo muhimu ya kuwaunga mkono, kama vile, fursa za masomo pamoja na vitendea kazi ambavyo vingewawezesha kuwa walimu bora wa elimu mjumuisho.

Walimu hawa mara nyingi wana uwezo na mawazo mazuri katika kufundisha lakini hawapati fursa za kubadilishana mawazo na walimu wengine au jamii. Vile vile, wazazi na jamii mara nyingi hawashirikishwi katika masuala ya kitaaluma na hawana uwelewa juu ya huduma, msaada na maarifa ambayo wangeweza kuchangia. Kwa ufupi, hakuna mashirikiano ambayo ni muhimu iwapo skuli na jamii zinatakiwa kuwa mjumuisho zaidi.

Kipindi hiki kinalenga kutoa uelewa juu ya majukumu muhimu ya waratibu wa elimu mjumuisho katika ngazi ya skuli na jamii kwa jumla.

Washiriki wataelewa kwamba, mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli hawajibiki kufanya kazi zote za elimu mjumuisho za skuli, badala yake kazi yake ni uratibu. Hii ina maana kwamba, atafanya kazi ya kuongoza na kusimamia Kamati ya Elimu Mjumuisho, wala si kwamba atakuwa na jukumu la kugundua, kutathmini na kuleta mambo yote mazuri ya Elimu Mjumuisho.

Kitendo cha 2.4a: Ni Nini Maana ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli?

Kikuu

Muda: Dakika 15

Kitendo hiki kitatoa fursa kwa kila mshiriki kufikiria na kujadili “ni nini maana ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli?”

Mkufunzi aeleze kuwa katika kitendo kilichopita **(Kitendo cha 2.3c)** majukumu ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli yameelezwa.

Mkufunzi awatake washiriki wafanye kazi kwa jozi na kujadili namna wanavyofahamu maana ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli. Kila jozi inatakiwa kuandika sentensi moja au aya fupi, kuelezea jinsi wanavyofahamu maana ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli.

Baadae, jozi zitabadilishana mawazo kwa ajili ya majadiliano. Mwisho vikundi vitatoa mrejesho wa kazi zao kwa kundi zima.

Baada ya kila mmoja kupata fursa ya kutoa mrejesho, mkufunzi ataandika maelezo yafuatayo, katika chati, ubao au bango.

“Mratibu wa skuli ana majukumu gani?”

Mratibu wa skuli anapaswa kutekeleza majukumu ya kiuratibu, hii ina maana kwamba ataongoza na kusimamia ili kuhakikisha kuwa utamaduni kamilifu wa mjumuisho, sera na utekelezaji wa Elimu Mjumuisho unapatikana skuli.

Kielelezonambari 2.8 **Ni yepi Majukumu ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli?**

Mkufunzi atawapatia washiriki **Kielelezo nambari 2.8.** Pia**,** maelezo haya yatawekwa ukutani ili yatumike kama rejea wakati wote wa mafunzo. Mkufunzi atawauliza washiriki iwapo wanataka kuongeza chochote katika maelezo hayo.

Mazingatio kwa Mkufunzi

Mkufunzi anapaswa kuzingatia kwamba chati au bango ambalo analotumia

liandikwe kwa usahihi kwa kutumia rangi nyeupe kwa weusi ili kuakisi mafunzo ya elimu mjumuisho.

Mkufunzi akumbuke kwamba, kama anatarajia walimu kuwa walimu wa Elimu Mjumuisho, anapaswa awe mkufunzi wa Elimu Mjumuisho. Njia nzuri ni kwa kila siku kutathmini mbinu anazotumia katika ufundishaji.

Kikuu

Kitendo cha 2.4b: Mchezo wa Nyekundu au Manjano (kubali au kataa)

Muda: Dakika 20

Mchezo huu utahamasisha majadiliano na utasaidia kuimarisha ufahamu wa washiriki kuhusu ni nani Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli?

Mkufunzi atawapatia washiriki kadi yenye rangi nyekundu na yenye rangi ya manjano, sawa na zile zinazotumiwa na muamuzi wa mpira wa miguu. Mkufunzi baadae atasoma maelezo kutoka kwenye **kielelezo nambari 2.9** na kumtaka kila mshiriki anyanyue kadi kutegemeana na kama anakubali au anakataa kuhusu maelezo yaliyotolewa.

- Kadi ya manjano ni **"kukubali"**
- Kadi nyekundu ni **"kukataa"**

Kielelezo nambari 2.9 **Maelezo kwa Ajili ya Majadiliano**

Baada ya kila maelezo kusomwa na kufanyiwa maamuzi, mkufunzi atoe nafasi kwa washiriki kujadiliana juu ya yale ambayo hawakukubaliana. Mkufunzi awahamasishe washiriki kujaribu kubadilishana mawazo na kusikilizana.

Mkufunzi hatalazimika kutumia maelezo yote. Anaweza kuchagua nukta tatu au nne za hoja ambazo anadhani kuwa ni muhimu katika kuwapatia washiriki uelewa wa kina juu ya majukumu ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli.

Kitendo hiki kimeandaliwa kwa ajili ya kuwahamasisha washiriki kutafakari majukumu ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli katika skuli na jamii zao. Hili ni jambo zuri kwa mkufunzi kwani linatoa muelekeo wa mawazo ya washiriki kuhusu Elimu Mjumuisho.

Ili kuona kwamba washiriki wameweza kukihusisha kitendo hiki na mazingira yao, mkufunzi amtake mshiriki mmoja kujitolea kusoma maelezo. Kufuatia

kitendo hiki, mkufunzi atabainisha na kutoa mrejesho juu ya njia ya uwasilishaji wa mshiriki aliyejitolea kama vile:

- Je walijadiliana kwa sauti kiasi ambacho kila mtu alisikia?
- Je kila mmoja alishirikishwa na kupewa fursa ya kuzungumza?
- Je walihakikisha kwamba kila mshiriki alisikiliza kwa makini wakati washiriki wengine walipokuwa wakijadiliana?

Kipindi cha 2.5: Sifa za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli

Utangulizi

Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli ni nafasi muhimu katika elimu hiyo. Ni muhimu kubaini aina ya mtu huyo ambaye angefaa zaidi katika jukumu hili na wala sio lazima mtu huyo kuwa na wadhifa wa juu au sifa nyingi za kitaalamu.

Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli lazima ajitolee kutoa fursa kamili kwa wanafunzi wote. Anapaswa awe mfano mzuri wa kuigwa, aliyetayari kusaidia na anayeweza kuwahamasisha wengine huku akielewa mahitaji ya wenzake, wanarika, pamoja na wanafunzi.

Kipindi hiki kitawasaidia washiriki kutafakari sio tu juu ya ujuzi utakaohitajika na Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli lakini pia sifa zake. Ni mtu wa aina gani anapaswa kuwa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli?

Kitendo cha 2.5a: Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli anahitaji kuwa…….?

Kikuu

Muda: Dakika 50

Mkufunzi awatake washiriki kupendekeza neno moja au maneno machache kuelezea kile wanachofikiria kuwa ni sifa za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli. Baadhi ya mifano itakuwa:

- Mpole
- Anayefikika
- Mtunza muda
- Rafiki na mtaalamu
- Muwajibikaji
- Aliye tayari kwa mabadiliko
- Mgunduzi
- Mfano mzuri wa kuigwa
- Mbunifu

Washirki wanahitaji kusema maneno machache tu na wala sio lazima kutoa maelezo yoyote kwani hayo yatashughulikiwa katika kitendo kinachofuata.

Kila pendekezo linapaswa kuandikwa kwa uwazi kwenye ubao au chati ikiwa washiriki wamemaliza na hawakutoa mapendekezo zaidi. Mkufunzi anapaswa kuangalia mawazo yao na kama kuna mapendekezo yao yoyote yaliyokosekana

anaweza kuyajumuisha katika chati.

Mkufunzi awagawe washiriki katika vikundi na kukipa kila kikundi maneno au sentensi mbili au tatu kutoka katika mapendekezo yao. Hakuna vikundi vinavyopaswa kuwa na mapendekezo sawa, idadi ya vikundi itategemea na idadi ya maneno na sentensi zilizopo katika chati.

Mkufunzi anaweza kutoa mfano mmoja, kama vile:

Kuwa na uwezo wa kushajihisha wengine kwa sababu walimu mara nyingi wanakuwa hawana muda au hawako tayari kutumia muda wao wa ziada kwa ajili ya mafunzo zaidi au kwa ajili ya kuandaa vielelezo. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anapaswa kulitatua tatizo hili kwa kuwashajihisha walimu zaidi.

Baadae, kila kundi watawasilisha mrejesho wa mapendekezo yao. Baada ya kumaliza zoezi hilo, mkufunzi atoe dakika chache kwa ajili ya kuwapa washiriki fursa ya kuuliza maswali na kutoa mawazo yao ya ziada

kielelezo nambari 2.10 Sifa za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli

Washiriki wapewe kielelezo nambari 2.10 na walinganishe mawazo waliyotoa na yale yaliyomo katika kielelezo.



Sifa za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli.

Kitendo cha 2.5b: Igizo dhima-Vitendo Vizuri na Vibaya

Kikuu

Muda: Dakika 90

Hili ni Igizo la kufurahisha ambalo huwapa fursa washiriki kuonesha sifa za Mratibu mzuri wa Elimu Mjumuisho wa skuli. Kazi ya kikundi itashajihisha mjadala na kubadilishana mawazo. Kama ilivyo katika vitendo vyengine, kikundi kitaelezea matumizi ya vifaa vya kufundishia vilivyotengenezwa kwa mali ghafi zinazopatikana katika maeneo yao.

Mkufunzi awagawe washiriki katika vikundi-ambapo idadi ya vikundi itategemea na idadi ya washiriki lakini mkufunzi anapaswa kuhakikisha kuwa kila kikundi kinaundwa na washiriki wasiopungua watano.

Kielelezo nambari 2.11 Matukio kwa ajili ya Igizo dhima

Kila kikundi Kipatiwe tukio moja kutoka katika **kielelezo nambari 2.11**. Kipatiwe dakika 15 za kujadili na kuonesha igizo lao. Baada ya dakika 15, kila kikundi kiwasilishe igizo lao ambalo halitatumia zaidi ya dakika 5.

Wakati washiriki wakiwa wanapanga maigizo yao, mkufunzi aandae chumba kwa ajili ya uwasilishaji, atayarishe sehemu kwa ajili ya jukwaa na apange viti kwa ajili ya hadhira.

Mwisho wa kila igizo dhima, washiriki watafakari na waamue iwapo Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli ana sifa zinazostahili zitakazopelekea ufanisi katika utekelezaji wa jukumu lake.

Mawazo yatawasilishwa kwa kutumia kadi zenye picha ya uso katika **kielelezo nambari 2.12.** Mkufunzi anapaswa kuziandaa kadi hizo kabla ya kipindi. Washiriki wataonesha kupitia igizo dhima, wanafikiria ni uso upi unaolingana na jukumu la mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli, kati ya uso unaoonesha hali ya furaha

☺ na ule wa hali ya kukasirika ☹.

Kielelezo nambari 2.12 **Muonekano wa Mtazamo wa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli**

☺ - Huyu ni Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli ambaye ana mtazamo unaokubalika na ni mtu sahihi.

☹ - Huyu ni Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli ambaye hakubaliki ingawa anaweza kufaidika kupitia mafunzo na ushauri

Mwisho wa igizo dhima kila kikundi kitapewa dakika chache kwa ajili ya majadiliano na maswali.

Mwisho wa vitendo hivi vya mwisho na kama kutakua na muda wa kutosha mkufunzi aandae kipindi juu ya mada inayoonesha kwa vipi Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli aweze kubadilisha vitendo vyake au tabia mbaya ili kuwa na ufanisi zaidi.

Washiriki wakiigiza juu ya vitendo vizuri na vibaya

[Maelezo ya picha: Mwanamme mmoja amekaa nyuma ya meza ndogo. Mbele yake katika nusu duara, kuna wanawake wanne na mwanamme mmoja. Nyuma kuna watu wawili ambao wanaangalia igizo dhima.]

Kipindi cha 2.6: Jukumu la Mtaratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli hati ndogo ziwe kubwa

Utangulizi

Mtaratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli ndie mtu muhimu anayehakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata fursa ya kujifunza na kufikia malengo kwa mujibu wa uwezo wa kila mmoja wao.

Mratibu huyu ndiye kiungo kikuu baina ya wanafunzi, familia, jamii, skuli na wataalamu wengine ambao wataunda mtandao kwa ajili ya kuzisaidia skuli jumuishi na jamii.

Lengo la kipindi hiki ni kujenga uelewa wa Elimu Mjumuisho na jukumu muhimu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli pamoja na kazi zake anapokuwa na Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli. Kufuatia kipindi hiki, washiriki wataelewa vipi skuli na jamii kwa ujumla zinaweza kuwekwa pamoja ili kuchukua majukumu na umiliki wa shughuli za Elimu Mjumuisho na kujivunia mabadiliko katika skuli zao. Washiriki wataelewa kuwa, Mratibu mzuri wa Elimu Mjumuisho wa skuli ana jukumu muhimu katika mchakato huo.

Kitendo cha 2.6a Namna Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli anavyoweza kufanya kazi katika Ngazi ya Jamii, Skuli na Wizara/Sera.

Kikuu

Muda: Dakika 40-45

Kitendo hiki kinahimiza washiriki kufikiria njia ambazo Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anaweza kuwa na ushawishi pamoja na ufanisi katika ngazi zote.

Mkufunzi awagawe washiriki katika vikundi vitatu. Ikiwezekana, kila kikundi kijumuishe wataalamu wa skuli, wasimamizi wakuu, walimu, wafanyakazi wengine wa skuli na mwanajamii au mfanyakazi yoyote kutoka katika ofisi za Wizara za Serikali, Taasisi binafsi n.k kama watakuwepo.

Mkufunzi aandike vichwa vya habari vitatu ubaoni au katika chati

- Skuli zenye Kamati za Elimu Mjumuisho.
- Jamii.
- Wizara ya Elimu katika ngazi ya sera.

Kila kikundi kati ya vikundi vitatu kipatiwe kimoja kati ya vichwa vya habari vya hapo juu na kutakiwa kubungua bongo na kuandaa uwasilishaji kuhusu namna Mratibu wa Elimu Mjumuisho anavyoweza kufanya kazi na (chombo/taasisi) hiyo.

Kwa mfano kikundi nambariri mbili (2) ni jamii. Uwasilishaji huu wa vikundi lazima uoneshe hatua mahususi jinsi Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anavyoweza kufanya kazi na kufaidika na ushirikishwaji wa skuli na jamii.

Ni muhimu kuwajulisha washiriki kuwa hakuna majibu sahihi au yasiyosahihi katika mazoezi haya. Jambo ambalo litafanya kazi vizuri katika skuli moja au jamii, huenda lisifanye kazi katika skuli au jamii nyengine. Wakati wa kujibu masuali ni lazima wafikirie **mbinu pacha** katika kujifunza. Pia, mazoezi haya yatawasaidia kufikiria mazingira yao wenyewe ya kazi.

Mwisho wa kila mawasilisho matatu, washiriki wapewe muda wa kufanya majadiliano ya jumla. Mkufunzi atumie **Kielelezo nambari 2.13** kuhakikisha kuwa mapendekezo yote yameandikwa na ambacho kimekosekana pamoja na kuweka mawazo yake. Mkufunzi aandike kwa uwazi nukta za mawazo ya nyongeza kwenye ubao au kwenye chati. .

Kielelezo nambari 2.13 **Mifano ya shughuli ambazo Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli anaweza kushiriki**

Mwisho, wapatie washiriki **kielelezo nambari 2:13** wasome.



Chati inayoonesha mawazo ya washiriki juu ya majukumu ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli ngazi ya jamii.





Chati inayoonesha mawazo ya washiriki juu ya majukumu ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli katika ngazi ya skuli.





Chati inayoonesha mawazo ya washiriki juu ya majukumu ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho katika ngazi ya Wizara.

[Maelezo ya picha: Picha za hapo juu ni chati mgeuzo zenye michoro na maneno yanayohusisha majukumu ya Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli.]

Kitendo cha 2.6b: Uratibu, Upangaji na Utekelezaji wa Ujumuishi

Kikuu

Muda: Dakika 90

Kitendo hiki kitawasaidia washiriki kuelewa ushirikiano unaopelekea mafanikio ya ujumuishi. Kwa kutumia "kisa mafunzo" washiriki watashajihishika kutafakari namna Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anavyoweza kuwaleta pamoja ili kubadilishana taarifa na ujuzi, upatikanaji wa huduma na upangaji wa mipango kwa ajili ya ujumuishi. Washiriki wataanza kutafakari juu ya jamii na mazingira yao ya kazi na kufikiria kuhusu watu watakaoweza kuwasaidia na kuwapa uelewa kwa ajili ya kutekeleza ujumuishi.

Kwa mara nyengine, ikiwezekana washiriki wanapaswa kuwa katika vikundi vitano mchanganyiko ili kila kikundi kiundwe na watu kutoka skuli, Kamati ya Elimu Mjumuisho, jamii, Wizara za Serikali na Taasisi zisizo za kiserikali.

Kielelezo nambari 2.14 Hadithi **ya Jabir**

Mkufunzi awasomee washiriki **kielelezo nambari 2.14** kinachohusu hadithi ya Jabir au amtake mshiriki yoyote kujitolea kusoma.

Kielelezo nambari 2.15 **Kufanya Kazi Kuelekea Ujumuishi**

Kila kikundi kipatiwe "kisa mafunzo" au picha kutoka **katika Kielelezo nambari 2.15** na kitakiwe kumjadili mwanafunzi au mazingira.

Lazima vikundi viandae mpango au orodha ya hatua kwa ajili ya ujumuishi, hatua ambazo kikundi kinadhani Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anapaswa kuchukua ili kuhakikisha mwanafunzi, mazingira na skuli zinakua jumuishi zaidi.

Mkufunzi aandike maneno "ushirikiano" na "uratibu" ubaoni kama ukumbusho kwa vikundi kuwa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli hawajibikiwi kufanya kazi zote na badala yake anapaswa kuchagua na kuwafanyia uratibu wengine ili

kushirikiana nao

Kisha, kila kikundi kiwasilishe mpango wa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli kwa ajili ya ujumuishi. Vikundi vioneshe mawasilisho yao katika chati juu ya kuta za chumba cha mafunzo. Kisha, Mjumbe mmoja kutoka kila kikundi, ataendelea na uwasilishaji wao. Washiriki wengine watazunguka chumbani ili kusoma kwa karibu zaidi kila wazo linalojadiliwa katika mpango na kuongezea kwa kuandika maoni na mapendekezo yao kwenye kila wasilisho. Mwishoni mwa kipindi hiki washiriki wote wanapaswa kuwa wameupitia kila mpango na kuwa na muda wa kutosha wa kuuliza masuali yanayohusu mpango huu. Wakati wa kitendo hiki mkufunzi anapaswa kuzunguka katika vikundi na kuangalia, kusikiliza na kutoa maelezo ya kina juu ya mambo mapya yaliyoongezwa na mapendekezo muhimu.

Vikundi vikiwasilisha mipango yao

Vikundi vikiwasilisha mipango yao

[Maelezo ya picha: katika picha zote mbili hapo juu, wanaume na wanawake wapo nje na wamejigawa vikundi vidogo vidogo, kila kikundi kimejikusanya karibu na chati mgeuzo iliyotundikwa ukutani.]

Kwa vile hiki ni kitendo kikuu katika kipindi hiki, ni muhimu kwa mkufunzi kubadilika na kutoa muda wa kutosha kwa ajili ya majadiliano na maswali. Kitendo hiki kinaangalia uwezekano wa kupata wadau na kwa namna gani watashirikishwa. Kwa hivyo, washiriki watahitaji muda wa kutosha kwa ajili ya kutafakari watu gani watashirikishwa na watafanya vitendo gani.

Mfano mwengine wa kitendo hiki utakuwa:

Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli ni mtu muhimu ambae amefahamishwa kuwa, mwanafunzi hawezi kusoma vizuri kwa sababu ana uoni hafifu. Hivyo anaweza kuwasiliana na wazazi au walezi pamoja na mhudumu wa afya wa mtaa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa macho yake. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli ahakikishe kuwa mwalimu anatoa msaada kwa ajili ya mikakati itakayopelekea ushirikishwaji mzuri wa wanafunzi (angalia moduli ya ziada juu ya **kuwashirikisha wanafunzi wenye mahitaji ya ziada (uk. 21)** kwa ajili ya mbinu zilizopendekezwa).

Mkufunzi lazima asisitize juu ya ukweli kwamba, mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli hafanyi na wala hawezi kufanya kila kitu. Yeye anaratibu kwa kushirikiana na watu wengine ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanajumuishwa.

Kitendo cha 2.6c: Kipindi cha Kikao cha Ziada

Zaida

Muda: Dakika 30

Iwapo muda wa ziada utapatikana mkufunzi ataandika ubaoni kichwa cha habari kitakachosomeka “ushirikishwaji”. Atawataka washiriki kufikiria kuhusu skuli na jamii zao na wajadili watu na mikakati kwa ajili ya ujumuishaji zaidi. Mkufunzi ataanza majadiliano kwa kutoa mifano kama vile;

Mzazi mmoja katika kijiji changu ni hodari sana katika kuisarifu miti na kwa kutumia miti hiyo anatengeneza vifaa vya kufundishia somo la hisabati na anakujanavyo skuli kwa ajili ya kutoa maelezo ya namna ya kutumia vifaa hivyo kabla ya mwalimu kuvitumia.

Mawazo mengine kwa ajili ya kuongoza majadiliano yanaweza kuwa:

- Kuunganisha baina ya mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli na makundi ya jamii
- Msaada kutoka kwa wazazi na ndugu wakubwa
- Msaada wa vikundirika kwa wanafunzi
- Msaada wa vikundirika na kushirikiana miongoni mwa walimu
- Uhamasishaji kupitia vyombo vya habari
- Jukumu la Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli katika moja ya miongoni mwa yaliyoainishwa hapo juu.

Nukta za hapo juu ni mapendekezo na sio lazima yajadiliwe, ni nukta za mwongozo ili kumsaidia mkufunzi kuwezesha majadiliano yaende vizuri. Washiriki watakuwa na mawazo na ushauri wao kwa ajili ya kushirikiana na skuli na jamii zao.

Kipindi cha 2.7: Mtazamo wa Skuli kwa Elimu Mjumuisho ni Jukumu la Msingi la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli

Utangulizi

Ili skuli iwe ya mjumuisho zaidi, elimu inayotolewa inapaswa kuakisi mazingira halisi ya wakati uliopo. Mambo mazuri yatakuwa yakipatikana kwa kila skuli. Baadhi ya mbinu za Elimu Mjumuisho zimekuwa na mafanikio na hazihitaji mabadiliko. Baadhi ya mikakati inaonekana sio jumuishi au haifanyiki kabisa na hapa ndipo ambapo skuli nzima inapaswa kufanya kazi kwa pamoja ili kuleta mabadiliko. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli atakuwa kama mshauri, mfuatiliaji na mtathmini, na kuwakumbusha wadau kuhusu umuhimu wa kutumia mbinu-pacha katika mfumo wote wa ujifunzaji.

Mwisho wa kipindi hiki, washiriki wataweza kuzingatia mawazo yatokanayo na vitendo walivyofanya ambavyo vitawasidia kuifanya skuli kuwa ya mjumuisho zaidi. Washiriki watapaswa kufahamu kwamba, Mratibu anaweza kushauri na kuisaidia skuli katika kufanya mabadilliko na kuzingatia kwamba mabadiliko yanayotokea ni jukumu la wote. Mratibu hawezi kutekeleza majukumu kama ya kwake binafsi.

Kitendo cha 2.7a: Shughuli za Mjumuisho ndani ya Skuli

Kikuu

Muda: Dakika 60

Maelekezo kwa Mkufunzi
Washiriki wataainisha vitendo vizuri ambavyo vimeshafanyika ndani ya skuli zao, sambamba na kubainisha maeneo ambayo yanahitaji kuimarishwa. Jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli ni muhimu katika kupanga na kusaidia utekelezaji wa mabadiliko hayo.

Mkufunzi anapaswa kuandika orodha ifuatayo katika chati.

- Mbinu za kufundishia na vitendo vya kujifunza.
- Mazingira
- Vitu vilivyomo ndani na vilivyoizunguka skuli

- Kuunganisha wazazi na jamii
- Usaidizi wa vikundi rika na urafiki kwa wanafunzi wote
- Uongozi wa skuli
- Uhamasishaji wa wafanyakazi wa skuli, wanaosomesha na wasiosomesha.
- Mafunzo ya ndani kwa walimu
- Mbinu pacha.

Mkufunzi agawe mada moja au mbili katika hizi kwa kila kikundi ili kila mada iwe imefanyiwa kazi. Huku wakifanya kazi kwa jozi katika vikundi vyao, washiriki wafikirie ni kwa namna gani skuli zao ni skuli za Elimu Mjumuisho na pia, waorodheshe skuli zao zinafanya vitendo na mikakati gani ambayo ni mizuri na ni ya mjumuisho inayohusiana na mada walizojifunza. Kwa mfano, kikundi kimoja kinaweza kupewa mada zinazohusu "mazingira" na njia za kufundishia na vitendo vya kujifunzia" mada. Kwa hivyo, washiriki watabadilishana mawazo katika jozi kama kwamba skuli zao zimejenga njia za mteremko kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji ya ziada.

Baadae washiriki watabadilishana mawazo katika vikundi vyao. Kisha, vikundi vitoe mrejesho wa mawazo yao kwa darasa zima, ambayo yanapaswa kuandikwa kwenye chati au ubao.

Washiriki wanapaswa kuchunguza orodha iliyoandaliwa na vikundi vyote. Kwa kuzingatia nukta za hapo juu, katika vikundi vyao wataamua ikiwa skuli zao ni za mjumuisho. Mawazo yao yanaweza kutumika kama mrejesho kwa vikundi vyote.

Kwa kuzingatia orodha iliyoandaliwa, mkufunzi awatake washiriki kufikiria ni kwa namna gani Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli huleta mabadiliko kwa ajili ya mjumuisho zaidi. Kwa njia ya jozi, washiriki watajadiliana kwa muda wa dakika 5-10. Baadaye kila kikundi kitachagua mada moja kutoka kwenye orodha na kuandaa mrejesho. Mada hizo ni 'Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anapaswa kufanya nini katika kuzisaidia skuli kuwa mjumuisho zaidi? Mkufunzi ahakikishe kuwa vikundi vinachagua mada tafauti.

Kwa mfano:

> Mratibu wa Elimu Mjumuisho katika skuli anachukua hatua gani kuhakikisha kuwa uongozi wa skuli una mwamko mkubwa juu ya elimu mjumuisho?

Au

> Mratibu wa Elimu Mjumuisho katika skuli anafanya nini kuhakikisha kuwa mbinu za kufundishia zinazotumika ni za mjumuisho?

Washiriki watatakiwa kutoa majibu yao kwa kutumia mbinu watakazo zichagua mfano njia ya mazungumzo, maandishi, michoro au picha zinazoelezea kazi za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli. Kumbuka kutumia moduli za ziada Kuwajumuisha **wanafunzi wenye mahitaji ya ziada** kama kielelezo kwa ajili ya maelezo ya ziada ikiwa yatahitajika.

Baada ya dakika 10 hadi 15 kila kikundi kitawasilisha mawazo yao. Muda utatolewa kwa ajili ya maswali na mapendekezo. Kazi za washiriki zitawekwa kwenye kuta ili kuwapa fursa washiriki kuongeza mapendekezo yao.

Kielelezo nambari 2.16

Wanafunzi, Wazazi au Walezi wanasema nini?

Mwisho mkufuzi awatake washiriki kusoma katika **kielelezonambari 2.16**.

Awaeleze kuwa hizi ni baadhi ya dondoo zilizoandaliwa na wanafunzi, wazazi au walezi wakati wa utafiti wa Elimu Mjumuisho katika programu ya mafunzo ya Elimu Mjumuisho kwa walimu, uliofanyika mwaka 2020. Katika utafiti huo, wanafunzi na wazazi au walezi waliulizwa wangefanya nini ili kuzifanya skuli zao kuwa za mjumuisho zaidi. Mkufunzi awatake washiriki kutafakari juu ya mapendekezo ya wazazi au walezi. Kama yapo wanayopendekeza, jee ni mapendekezo yepi yanayofaa kwa washiriki katika mazingira ya skuli zao? Je kuna dondoo miongoni mwa zile zilizowasilishwa ambazo ni za kushangaza? Kwa nini? Washiriki wanapaswa kutoa mrejesho wa mawazo yao kwa vikundi vyote.

Kitendo cha 2.7b: Shughuli za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli katika Skuli na Jamii.

Kikuu

Muda: Dakika 90

Maelekezo kwa Mkufunzi

Lengo la kitendo hiki ni kuwasaidia washiriki kupata uelewa kuhusu jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli katika skuli na jamii.

Mkufunzi atapaswa kuelezea kwamba baadhi ya wakati Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anaweza kupendekeza mawazo mapya na mbinu za kisasa katika kuleta ujumuishi wenye ufanisi, hata hivyo, mara nyingi mawazo yanapaswa kutoka skuli na jamii inayoizunguka.

Mkufunzi anapaswa kuandika vitendo vifuatavyo kwenye ubao au katika chati na kuelezea kwamba hivi ni vitendo ambavyo vinapaswa kufanywa na skuli au jamii katika kuifanya skuli jumuishi zaidi.

- Siku ya ufunguzi wa mjumuisho - Jamii na skuli.
- Programu za ushauri na kuvisaidia vikundirika - ushirikiano miongoni mwa walimu.
- Kuyafikia mazingira yanayozunguka - Skuli na jamii.
- Kuwepo majadiliano ya vikundi vya jamii pamoja na wanajamii wanaojitolea mfano, wanaojihusisha na kurekebisha tabia na wanaojihusisha na ukuzaji wa maendeleo jumuishi ambao wanatafuta njia mbali mbali za kutambulika kwa ujumuishi.
- Mpango wa kuwasaidia wanafunzi katika kipindi cha mpito - wadau kufanya kazi kwa mashirikiano
- Kutumia ujuzi na rasilimali zinazopatikana katika jamii - wahusika ni skuli na jamii

Washiriki wapatiwe dakika chache kutafakari juu yakitendo hiki. Wanaweza kuongeza michango mipya ya mawazo yao katika orodha ya mawazo yaliyohusu mjumuisho

Kielelezo nambari 2.17 **Igizo dhima la Mratibu wa Elimu Mjumuisho katika Skuli**

Mkufunzi atoe kadi za igizo dhima zilizonakiliwa kutoka katika **kielelezo nambari 2.17** kadi moja kwa kila kikundi kwa ajili ya kuandaa igizo fupi.

Vikundi vitachagua mshiriki mmoja ambaye aigize jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli na vitapewa dakika 15 hadi 20 kuandaa na kuwasilisha igizo dhima. Mkufunzi atakuwa akivizungukia vikundi na kutoa ushauri na msaada pale utakapo hitajika. Kila igizo dhima lisizidi dakika 5.

Mkufunzi awakumbushe washiriki baadhi ya mbinu za mjumuisho zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa uwasilishaji. Mfano; kuzungumza kwa uwazi. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila mshiriki anaona vizuri na anasikiliza kwa makini wakati washiriki wengine wanapozungumza. Kila sehemu ya uwasilishaji iliyoandikwa inapaswa kuwa yenye kuonekana vizuri iwe ya rangi nyeupe kwa weusi.

Wakati washiriki wanapopanga igizo lao, mkufunzi anapaswa kutayarisha chumba kwa ajili ya igizo, abainishe eneo kwa ajili ya jukwaa na apange viti kwa ajili ya hadhira.

Kila kikundi kinapaswa kuonesha igizo lao kwa kundi lote. Mwisho wa igizo dhima washiriki wapatiwe muda kwa ajili ya michango na masuali.

Igizo dhima

[Maelezo ya picha: Wanawake watatu (3) na wanaume 3 wamekaa kuzunguka duara. Mwanamke mmoja (1) amesimama na ameshika kitabu cha kumbukumbu huku washiriki wengine wakimuangalia akiwa anazungumza.]

Kipindi cha 2.8: Kuanzisha na Kuvibadilisha Vituo Saidizi vya Ujifunzaji ili kupelekea Ufanisi katika Ujumuishi

Utangulizi

Mabadiliko kutoka Elimu Maalumu kwenda Elimu Mjumuisho ni suala ambalo halijitokezi kwa mara moja. Ni mchakato wa muda mrefu, iwe kwa nchi zilizoendelea au zinazoendelea. Baadhi ya wanafunzi siku zote huhitaji msaada wa wataalamu ili kuweza kushiriki na kufikia malengo yao waliyojipangia. Mafunzo kazini lazima yawe endelevu ili kukuza ujuzi wa kitaaluma kwa baadhi ya walimu na kutoa mbinu za ujumuishi kwa walimu wote.

Katika kipindi hiki washiriki watakuwa wakijadili kuhusu matumizi ya vitengo vya elimu ya wenye mahitaji maalumu, madarasa maalumu n.k, katika kuziingiza skuli kwenye mabadiliko ambayo yatazipelekea kwenye kujihusisha na ujumuishi zaidi.

Vituo Saidizi vya Ujifunzaji: Ni vituo rafiki, vyenye mazingira tulivu, ambapo Waratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli, walimu na wafanyakazi wengine wanaweza kuvitumia kwa ajili ya upangaji na maandalizi, tathmini, mikutano na uungaji mkono wa mtu mmoja mmoja.

Washiriki watajadili na kubadilishana mawazo juu ya namna gani vituo vya elimu ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu vinaweza kushughulikiwa ipasavyo na kutumika kama vituo saidizi vya ujifunzaji na kujadili jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli katika kufanya mabadiliko na kuandaa masuala ya baadae katika vituo hivyo.

Taarifa za ziada zinapatikana katika moduli ya ziada juu ya: **kuwajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu**, katika moduli hiyo tunaweza kupata rejea muhimu.

Kitendo cha 2.8a: Uundaji wa Vituo Saidizi vya Ujifunzaji ndani ya Skuli

Kikuu

Muda: Dakika 60

Mwisho wa kipindi hiki, washiriki wataeleza uwezekano wa kuvibadilisha vitengo vya elimu ya mahitaji maalumu na kuwa jumuishi zaidi kama vituo saidizi vya ujifunzaji. Washiriki watabadilishana mawazo juu ya namna ambayo vituo saidizi vya ujifunzaji vinaweza kutumika kusaidia ujumuishi.

Mkufunzi awasilishe utangulizi wa kipindi hiki (angalia juu) na kisha awapatie washiriki **kielelezo nambari 2.18.** Aelezee kwamba mapendekezo yaliyomo katika nakala hiyo yamejikita katika modeli za nchi nyengine na hivyo zinapaswa kubadilishwa ili yaendane na mazingira ya Zanzibar.

Kielelezo nambari 2.18 **Kutumia Vituo Saidizi vya Ujifunzaji Kiufanisi**

Mkufunzi abainishe kwamba baadhi ya mapendekezo yaliyoorodheshwa hapa tayari yameshaanza kujitokeza na kufanyiwa kazi Zanzibar, kwa mfano:

- Uendelezaji na kuwepo kwa madarasa ya kuhifadhia vifaa
- Sehemu za kufanyia kazi Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli
- Kufanyika mikutano ya wazazi au walezi

Kisha, washiriki watagaiwa katika vikundi. Mkufunzi atoe dakika 30 kwa ajili ya mjadala wa vikundi juu ya mada hii, vile vile, juu ya jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli huku akihusisha na vituo wezeshi vya ujifunzaji. Vikundi viandae maelezo mafupi na viorodheshe hoja za msingi juu ya mabadiliko ya vitengo vya mahitaji maalumu ya elimu kwenda kwenye vituo saidizi vya ujifunzaji jumuishi.

Wakati wa mjadala katika vikundi, mkufunzi ahakikishe kuwa, kila mmoja anapata fursa ya kuchangia. Avipitie vikundi kwa ajili ya kuviangalia na kuvichunguza. Akikumbushe kila kikundi pia, kutafakari juu ya jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli katika kila mchakato.

Mwisho wa majadiliano katika vikundi, muwasilishaji kutoka kila kikundi awasilishe hoja muhimu zilizojadiliwa, huku akitoa ufafanuzi kwa ufupi. Mkufunzi aziandike hoja kuu zote juu ya ubao au chati. Kama itawezekana, vikundi vieleze mapendekezo yao yote juu ya jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli.

Matokeo ya vitendo hivi yanapaswa kuwa ni kupatikana kwa mchoro au orodha inayoakisi mawazo ya mabadiliko na matumizi ya vituo wezeshi vya ujifunzaji vyenye ufanisi.

Kazi za Vitendo za Skuli

Mkufunzi awatayarishe washiriki kwa ajili ya kazi za vitendo za skuli. Kazi ambazo watahitaji kukamilisha kabla ya kurejea kwa ajili ya warsha inayofuata ya mafunzo ya wakufunzi. Kazi zenyewe ni:

- Kuhakikisha timu ya ujumuishi ya skuli imeundwa katika skuli yako ya majaribio.
- Kuhakikisha kuwa walimu, Maafisa Elimu wa Wilaya, na wanajamii wanajua nani anafaa kuwa mjumbe wa kamati, kwa nini inaundwa kamati ya ujumuishi ya skuli na ni yepi majukumu yake. Jadili kuhusu ujumuishi na Kamati ya ujumuishi ya skuli na umuhimu wa **kuwepo kwake**, **ushiriki** na mafanikio yake
- Kuainisha uwezo wa Mratibu wako wa Elimu mjumuisho katika skuli yako.
- Kuainisha vituo saidizi vya ujifunzaji vinavyoweza kutumika katika kila skuli.
- Kumsaidia Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli kufanya yafuatayo: -
    - Kuandaa mikutano itakayolenga kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu kazi inayoendelea ya elimu mjumuisho.
    - Kuhakikisha kuwa walimu wote wanaofanya kazi kama waratibu wa elimu mjumuisho wa skuli wanafahamu majukumu yao katika skuli.
    - Kuwapatia mafunzo walimu wapya kuhusu elimu mjumuisho na ujumuishi katika skuli.
    - Kupanga na kuandaa mkutano wa kamati ya elimu mjumuisho na jamii

kuhusu jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho.

Washiriki wanapaswa kutekeleza kazi hizi pamoja na Kamati ya Elimu Mjumuisho. Wanalazimika kuhakikisha kuwa wanaweka kumbukumbu ya mchakato na muendelezo wa kazi hizi na kutafakari juu ya ni kipi kinachoendelea vizuri au kisichoendelea vizuri. Washiriki wanapaswa kuainisha njia za kuimarisha na kukuza vitendo ambavyo havikwenda vizuri. Nukta hizi za maelezo na mrejesho wake zitajadiliwa kwenye warsha ya mafunzo ya wakufunzi.

Vielelezo

Moduli

2

Kielelezo nambari 2.1: Kisa Mafunzo cha Kamati ya Skuli ya Mjumuisho

Kufanya kazi pamoja kwa ajili ya mjumuisho: mfano wa kamati ya skuli ya mjumuisho nchini Macedonia

Dimo Hadzi Dimov School, Skopje, Macedonia, wajumbe wa Kamati ya Elimu Mjumuisho.

Walimu wengi wana wasiwasi juu ya namna ya kufanya madarasa yao kuwa mjumuisho ipasavyo.

Kuna baadhi ya walimu wanahisi kuwa hawana ujuzi unaotakiwa ambao utawafanya kuwa sehemu ya mjumuisho. Hili haliepukiki - mwalimu mmoja hawezi kuelewa na kufanya kila kitu mwenyewe. Hii ndio sababu ujumbe muhimu wa muongozo au vifaa vya mafunzo vya Elimu Mjumuisho mara zote huwa ni: ''Fanya kazi pamoja na wenzako na wadau wakusaidie kubaini na kutatua changamoto za mjumuisho." Katika Makala hii, walimu katika skuli ya Dimo Hadzi Dimov, Skopje, iliopo Macedonia, wanaelezea namna ambavyo timu ya skuli ya mjumuisho humsaidia kila mmoja kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuzifanya skuli zao kuwa rafiki kwa watoto na mazingira ya mjumuisho.

Historia

Skuli yetu ilikuwa na timu ya skuli ya mjumuisho tangu mwaka 1998 - baadhi ya washiriki wamekuwa ni wanakamati tangu ilipoanzishwa. Ilikuwa wakati huo ambapo UNICEF walitambulisha na kuanzisha mradi juu ya mjumuisho wa Watoto wenye mahitaji maalumu ya kielimu katika skuli za kawaida. Ilikuwa siku zote sera ya skuli ni kuwachukuwa watoto wote, bila ya kuzingatia walipotoka. Hii haimaanishi kwamba tulijuwa kila kitu kuhusu Elimu Mjumuisho tangu siku ya mwanzo.

Sera ya mjumuisho imeendelea kuwepo kwa muda mrefu katika skuli yetu; mazingira yetu chanya ya kukubali ndio matokeo ya mchakato wa muda mrefu wa kujifunza na kujibadilisha. Vile vile, tulishajihisha kupata mashirikiano na walimu wa madarasa, walimu wa masomo na wazazi.

Kuwa na mashirikiano thabiti na uongozi wa skuli katika kipindi hiki ilikuwa ni jambo muhimu sana. Dira ya mwanzo kwa mjumuisho ilikuja kutoka

kwa Mwalimu mkuu. Tumekuwa na viongozi wanne tangu tulipoanza timu ya mjumuisho, pale ambapo kiongozi mpya anajiunga tunahakikisha kuwa tunamwambia kuhusu mjumuisho na tunamshirikisha mara moja katika juhudi zetu za kuimarisha mjumuisho, hivyo anaweza kujionea kazi nzuri ambayo ilikuwa tayari inaendelea na anakuwa na furaha kusaidia ili kuhakikisha kazi hiyo inaendelea mbele.

Wajumbe wa Kamati

Mwanzo tulianza na kamati yenye walimu watatu wa madarasa, mwalimu mkuu mfundishaji na mwanasaikolojia. Ingawa kamati ilikuwa inaonesha mabadiliko ya ujumuisho wa wanachama wake; kila siku ipo tayari kuendelea kubadilika iwapo itahitajika. Baadhi ya wanachama hujiunga na kutoka baada ya muda fulani, baadhi hukaa kwa muda mrefu, baadhi ya wanachama ni wataalamu kutoka nje na wazazi. Mara nyingi muundo halisi hutegemea mpango wa utekelezaji tulionao kwa kipindi fulani, na huo ndio msukumo tunaouhitaji katika kamati, nje ya wajumbe wa kawaida.

Matarajio Makubwa

Ni lazima kwa walimu wote katika skuli yetu kujifunza kuhusu elimu mjumuisho, kwa kupitia warsha na ushauri. Ikiwa tunataka mabadiliko yatokee basi kila mmoja katika skuli anatakiwa apewe taarifa – haitasaidia kitu ikiwa walimu wachache ndio wanafahamu kuhusu mjumuisho. Tunataka skuli nzima ipate hadhi ya maendeleo makubwa ya kitaalamu, kupania kujifunza zaidi na kujiimarisha sisi wenyewe. Ingawaje sisi ni watu wazima na walimu wenye sifa lakini bado tunaweza kujifunza zaidi. Kwa mfano, kwa miaka ya hivi karibuni baadhi ya wajumbe wa kamati wamelenga kujifunza zaidi katika kuwabaini watoto wenye vipaji vikubwa, kwani wanaweza kutengwa ikiwa matakwa yao ya masomo hayatofikiwa.

Pale walimu wapya wanapoajiriwa, kamati ya skuli ya mjumuisho haina uwezo wowote wa kudhibiti mchakato wa kutangaza na kusaili, kwa hivyo, kukubali elimu mjumuisho sio sehemu ya mchakato rasmi wa uteuzi lakini pale walimu wapya wanapoanza kazi, tunawaonesha tunamaanisha nini kuhusu mjumuisho na yepi matarajio ya skuli yetu. Tunafanya hivi kupitia ushauri na uungwaji mkono kutoka kwa mtu mmoja mmoja. Ni moja kati ya kazi zetu kama wajumbe wa kamati ya skuli ya mjumuisho kuwakagua walimu wenzetu na kuwasaidia wanapokuwa na matatizo juu ya ujumuishi. Mwanzo baadhi ya walimu walikuwa wanasita lakini wanapowaona walimu wengine wanavyofanya kazi pamoja na kusaidiana kupanga kazi zao, hutaka kujiunga.

Kushirikisha Walimu Wote

Tulipokuwa tunaanzisha kamati miaka 13 iliyopita, tulikuwa tukifanya kazi sana na walimu wa madarasa wanaosomesha katika kiwango 1-5, ngazi ya msingi chini lakini taratibu tukaanza kuwasaidia walimu wa masomo wanaofanya kazi katika madarasa ya ngazi ya msingi ya juu (kiwango 6-9). Pia, tulihakikisha kuna mchakato wenye ufanisi wa kukabidhiana kati ya msingi chini na msingi juu, mtoto mwenye mahitaji maalum anaendelea kupata kiwango na ubora ule ule wa huduma kadri wanavyosonga mbele katika viwango vya juu.

Hata hivyo, sasa hivi tunakabiliana na changamoto ya kuhakikisha ni kwa namna gani watoto hawa wanapata msaada wanapoondoka skuli zetu za msingi na kujiunga na skuli za sekondari, sio kila skuli za sekondari ni mjumuisho na kwamba zinawasaidia ipasavyo. Kwa vile baadhi yao wanaitwa 'wanafunzi wenye mahitaji maalumu' huwa wanakwenda vyuo vikuu au kushindana katika michezo ya olimpiki ya watoto wenye ulemavu kwa bahati mbaya wengine wakifika sekondari wanashindwa kuendelea mbele. Hili ni tatizo ambalo tunatakiwa kulitatua na ni jambo ambalo hatutoweza kukabiliana nalo sisi wenyewe kama walimu wa skuli za msingi.

Utambuzi wa Mahitaji ya Watoto

Kabla ya watoto kuwasili skuli kwa siku ya mwanzo, tunatumia muda kuwafuatilia, kwa hivyo tunapata mawazo ya mwanzo ya mahitaji yao ya kusoma, hamu na uwezo wao. Wakati wanajiandikisha tunatumia muda kuandika muundo mzuri wa madarasa, ili kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalumu wanawekwa na walimu wenye ujuzi mzuri ili kuwasaidia. Walimu wote wana watoto wenye mahitaji maalumu katika madarasa yao, ingawaje, si vizuri kuwaacha watoto wenye changamoto za kujifunza kwa walimu wachache walio tayari kuwafundisha, unahitajika mchakato maridhawa wa kulinganisha mahitaji ya kujifunza na ustadi wa kufundisha.

Kufanya kazi kwa ushirikiano

Kama ni walimu tunafanya kazi kwa ushirikiano. Mwalimu mkuu, wakufunzi na wanasaikolojia wanashiriki katika kuwasimamia walimu. Pia, tuna madarasa ya wazi ambapo wenzetu wa kamati wanaweza wakakaa na kutizama walimu wanavyosomesha. Tunakuwa pamoja kwa muda wote, kulinganisha maelezo na uzoefu, kulingana na wanafunzi wetu wote, sio kama wote watakuwa na mahitaji maalumu. Kamati ya Elimu Mjumuisho husaidia kuwezesha ushiriki huu. Kamati pia hutoa mafunzo kwa walimu katika skuli nyingine, chini ya mamlaka ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Kitengo cha Maendeleo

ya Elimu.

Kamati yetu huwahamasisha walimu kuhakikisha kwamba watoto katika skuli yetu wanafanya kazi kwa pamoja, wanashirikiana na kusaidiana kupitia kusoma kwa vikundi. Tunawasaidia walimu kutumia mbinu shirikishi za kufundishia na kujifunzia. Hakuna kutumia njia ya mihadhara. Mbinu hizi husaidia kutoa mrejesho zaidi kutoka kwa wanafunzi, na inavutia zaidi kwa kila mmoja. Masomo yanayohusisha wanafunzi kufanya vitu kwa mikono yao na sio tu kuzungumza na kuandika.

Tunahakikisha kuwa tuna uhusiano mzuri na wazazi ambapo hujihisi wanashirikishwa vyema katika juhudi za Elimu Mjumuisho. Tunawafikia na kuwaeleza kuhusu mjumuisho, na tunawashirikisha katika michakato ya upangaji wa mipango binafsi kwa ajili ya watoto wao.

Pia, tunafanya kazi kwa ushirikiano na skuli nyingine, kufanya kile tunachokiita 'Darasa mchanganyiko' ambapo madarasa kutoka skuli mbili tafauti yanaungana kusoma kwa pamoja. Ikiwa hili linatokea kamati yetu ya elimu mjumuisho ya skuli huwasaidia walimu kupanga mahitaji ya vifaa vya kusomea kwa watoto wote wa darasa lililochanganywa. Hii pia inamaanisha kuwa walimu na watoto kutoka skuli nyengine wanapata uzoefu wa namna tunavyofanya kazi kuelekea katika kufanya vitendo zaidi vya mjumuisho katika skuli yetu.

Ni nini kinachofuata?

Kwa sasa hatuna majibu yote. Bado tunakumbana na changamoto nyingi. Tunajitahidi sana kupanga masomo ya kila mtoto kwa ufanisi lakini hatujafanikiwa, kwa hivyo, tunahitaji msukumo zaidi katika baadhi ya maeneo ya kazi, kama vile kuendeleza na kukuza mipango binafsi ya elimu. Na tunajua kwamba sio watoto wote wanaendelea kupata maendeleo mazuri wanapokuwa wameondoka katika skuli yetu, kwa sababu skuli nyingine wanazokwenda zinakuwa hazijaandaliwa vizuri. Kwa hivyo, tunahitaji msaada kutoka nje ya skuli yetu kuhakikisha kwamba mjumuisho sio kitu kinachopaswa kuwepo katika skuli chache tu.

Kielelezo nambari 2.2: Mbinu pacha

Elimu mjumuisho inalenga kubadilisha mfumo na sio kumbadilisha mwanafunzi. Hata hivyo, kwa kuzingatia mabadiliko ya kiwango cha mfumo, haimaanishi kwamba tunapaswa kupuuza mahitaji mahususi ya kila mwanafunzi. Tunahitaji kukabiliana na mitazamo ya kutotiliwa maanani kwa Elimu Mjumuisho katika namna mbili: Namna hizo ni kuimarisha mabadiliko ya kimfumo na kwa kutoa msaada maalumu kulingana na mahitaji ya kujifunza kwa kila mwanafunzi. Hii ndio inaitwa mbinu pacha.



Kielelezo nambari 2.3: Ufupisho wa Kamati ya Elimu Mjumuisho

Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli:

- Inawaleta watu pamoja ambao wana majukumu katika elimu au katika skuli yao na ambao lengo lao ni moja ambalo ni la kuifanya skuli kuwa mjumuisho zaidi.
- Ina wajumbe na uwakilishi mpana unaoundwa na watu wanaojitolea
- Ipo kwa ajili ya **kuwasaidia** walimu, wafanyakazi wengine wasiokuwa walimu, wanafunzi na wazazi au walezi na sio kuongeza tabaka jengine la urasimu au mzigo. Ikiwa kamati inakuwa mzigo au chombo cha urasimu, kama hivyo, haitofanya kazi kama ilivyokusudiwa.
- Kuwa mfano mzuri wa kueleza juu ya nini maana ya mjumuisho katika uhalisia wake na husaidia kutoa msaada wa kivitendo na ushauri kiasi ya kwamba hubadili elimu ya nadharia ya mjumuisho kuwa ya uhalisi na vitendo.
- Hushughulikia masuala yote ya Elimu Mjumuisho katika skuli ambayo yanaweza kutokea katika vipindi tafauti katika mwaka wa masomo. Kwa mfano, sababu na masuluhisho katika matukio ya ugomvi, kupigana, maonevu mbali mbali, utoro na uchelewaji ambazo ni miongoni mwa changamoto zinazojitokeza katika skuli za mjumuisho.

Kielelezo nambari 2.4: Kisa Mafunzo – Maana ya Kamati ya Skuli ya Mjumuisho?

Washiriki wapatiwe maneno yaliyopo kwenye sanduku

Soma visa mafunzo hivi. Unafikiri kila kisa mafunzo kinaelezea Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli? Kwanini?

- Ina wajumbe na uwakilishi mpana unaoundwa na watu wanaojitolea
- Ipo kwa ajili ya **kuwasaidia** walimu, wafanyakazi wengine wasiokuwa walimu, wanafunzi na wazazi au walezi na sio kuongeza tabaka jengine la urasimu au mzigo. Ikiwa kamati inakuwa mzigo au chombo cha urasimu, kama hivyo, haitofanya kazi kama ilivyokusudiwa.
- Kuwa mfano mzuri wa kueleza juu ya nini maana ya mjumuisho katika uhalisia wake na husaidia kutoa msaada wa kivitendo na ushauri kiasi ya kwamba hubadili elimu ya nadharia ya mjumuisho kuwa ya uhalisi na vitendo.
- Hushughulikia masuala yote ya Elimu Mjumuisho katika skuli ambayo yanaweza kutokea katika vipindi tafauti katika mwaka wa masomo. Kwa mfano, sababu na masuluhisho katika matukio ya ugomvi, kupigana, maonevu mbali mbali, utoro na uchelewaji ambazo ni miongoni mwa changamoto zinazojitokeza katika skuli za mjumuisho.

Kisa mafunzo A
Mara moja kila baada ya miezi 3, walimu watatu wa darasa la skuli ya kijijini wanakaa pamoja na kujadili matatizo yanayowakabili katika kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu walioandikishwa skuli. Walimu wegine wawili katika skuli hawataki kuhudhuria kwenye mikutano hii na hakuna aliyewahamasisha kufanya hivyo.

Kisa mafunzo B
Kwenye skuli kubwa, kamati imeundwa kwa ajili kuandaa mipango binafsi ya kielimu kwa wanafunzi 30 waliotambuliwa kuwa na mahitaji maalumu ya kielimu. Kamati imeundwa na mkufunzi, inajumuisha mtaalamu wa mbinu za ufundishaji, mwanasaikolojia, walimu 2 wa darasa na walimu 3 wataalamu wa elimu maalum kutoka nje ya skuli.

Kisa mafunzo C
Mara moja kwa mwaka, skuli C huwaita wazazi au walezi kuhudhuria mkutano. Katika mkutano huu, mwalimu mkuu huwaelezea wazazi, walezi au waangalizi kuhusu sera ya skuli juu ya Elimu mjumuisho, akiwataka kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanakwenda skuli, na kuwaambia kuhusu namna gani walimu na wafanya kazi wenye utaalamu wanawasaidia wanafunzi waliotambuliwa kuwa wana mahitaji maalumu ya kielimu.

Kisa mafunzo D
Skuli D ina vikundi mchanganyiko vya wanafunzi wenye mahitaji ya ziada ya kielimu wakiwemo wanafunzi wenye ulemavu, kikundi cha wanafunzi wenye changamoto za kitabia, wenye kuzungumza lugha tatu tafauti na vikundi vyenginevyo. Kikundi cha walimu, wazazi, walezi au waangalizi na wataalamu hukutana kwa baada ya wiki kujadili changamoto mpya za elimu mjumuisho zilizojitokeza na kuzitatua pamoja na kukagua maendeleo ya elimu. Ambapo kwa sasa wanachagua wanafunzi wawili kuwakilisha kikundi chao ili kutoa nguvu zaidi kwa wanafunzi wenzao na kusaidia kuwajuwa wanafunzi ambao hawahudhurii skuli.

Nukta za Maelezo ya Majibu yanayotarajiwa, Kumuongoza Mkufunzi kuwezesha zoezi hili.

Kisa cha mafunzo A: Je hii ni Kamati ya Skuli Mjumuisho?

- Ndio… kwa sababu hakuna muundo maalumu kwa ajili ya wanachama wa kamati au ni kwa muda gani hukutana mara ngapi, kwa hivyo, hakuna shaka, kwa mfano, kwamba kamati haina mtaalamu (labda skuli haina mkufunzi au mwanasaikolojia) au mtaalamu wa nje, au hukutana mara nne tu kwa mwaka.
- Hapana… kwa sababu kamati inaonekana kushughulikia watu wenye ulemavu na hususan wanafunzi maalumu kuliko kuwa na masuala ya kimfumo na sio kutazama upeo mkubwa wa changamoto za mjumuisho. Mfano, vijijini kunakuwa na matatizo ya umasikini mkubwa mno, usafiri wa kwenda skuli nakadhalika
- Hapana… hakuna jitihada ambayo imefanywa kuwajumuisha walimu wengine na pengine hakuna kilichofanywa katika kuongeza ufahamu wa Elimu Mjumuisho.

Kisa mafunzo B: Je hii ni Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli?

- Hapana… kwa sababu makusudio ya kamati ni finyu sana. Inaandaa mpango binafsi wa kielimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu. Haioneshi kama inafanya kazi kwa upana kwa maswala ya mjumuisho kwa wanafunzi hawa au wanafunzi wengine wanaokumbana na vikwazo vyengine vya kielimu
- Hapana….. kwa sababu wanachama ni zaidi ya wataalamu, sio wa kawaida, walimu mjumuisho na wadau wengine.

Kisa mafunzo C: Je hii ni Kamati ya Elimu Mjumuisho?

- Hapana… kwa sababu ingawa kuna ushirikishwaji wa wazazi au walezi na waangalizi lakini hakuna mashirikiano. Wazazi au walezi huwa wanaambiwa tu kilichotokea, lakini huwa hawaalikwi kushughulikia kikamilifu katika vitendo vya skuli mjumuisho kulijuwa tatizo na kulitatua.

Kisa mafunzo D: Je hii ni Kamati ya Elimu Mjumuisho?

- Ndio… kwa sababu kwa kiasi kikubwa inahusisha wadau wengi na kushughulikia masuala mbali mbali ya ujumuishaji.

Kielelezo nambari 2.5: Uhusiano wa Madaraka.

Kuna vyanzo tafauti vya madaraka au masuala mengine katika maisha yanayowapa watu madaraka ambayo sisi binafsi yanatukuta ama kwa kujua au bila ya kujua. Kwa mfano:

- Maarifa, uzoefu wa kazi, cheo na uwezo.
- Stadi za kusikiliza, nafasi ya uongozi na ushawishi wa mtu binafsi.
- Stadi za uchambuzi, udhibiti wa rasilimali na uwezo wa kutatua matatizo.

Madaraka yanaweza kuwa ya mtu binafsi au ya pamoja, kama maelezo yafuatayo yanavyoonesha:

“Madaraka” ni uwezo wa kueleza malengo binafsi na kuwashawishi wengine kuyafikia malengo hayo. Ni uwezo wa kupata tunachokitaka, kushikilia tunachokipata na kutengeneza matukio namna tunavyotaka kuyatengeneza.”

“Katika kiwango cha pamoja, madaraka ni uwezo wa kukusanya vyanzo tafauti vya nguvu binafsi kwa ajili ya kuleta hamu ya mabadiliko ambayo itanufaisha kikundi kizima kuliko mtu binafsi.”

Madaraka yanaweza kugawanywa katika aina 4 tafauti, nazo ni:

Madaraka makubwa: wengi wanajaribu kuongeza nguvu binafsi wakijaalia kwamba madaraka yana kikomo ikiwa mtu binafsi au kikundi hupata madaraka zaidi, wengine hupata kidogo.

Madaraka ya mtu binafsi: aina hii ya madaraka yanamaanisha suala la mtu binafsi katika **kumuwezesha** kimaslahi, inamuwezesha mtu kudhibiti au kusimamia hali kwa faida yake binafsi.

Madaraka ya pamoja: haya yanahusisha **madaraka ya pamoja** na yanaonekana pale ambapo kikundi kinashirikiana kutatua matatizo kwa pamoja na kutengeneza uwezo wa kufanya jambo ambalo ni kubwa zaidi kuliko kama likifanywa na mtu mmoja mmoja.

Madaraka ya ndani: madaraka ya aina hii yamo ndani ya mtu binafsi na uwezo wake mwenyewe. Inalenga katika **kujikubali** na **kujiheshimu mwenyewe**, ambapo hupelekea kuwaheshimu na kuwakubali wengine kwa

usawa ambapo baadae huyatanuwa kwa kuwakubali na kuwaheshimu wengine kwa usawa.

Madaraka ya juu ni namna ya vile tunavyoyaona madaraka.

Kawaida tunakadiria iwapo mtu au kikundi kwa pamoja wanakuwa na uwezo katika uhusiano, wengine wanapaswa kuwa na uwezo mdogo wa uhusiano, ambapo wengine huwa na nguvu kidogo. Tunategemea kwamba iwapo mwenye uwezo mdogo na atapata nguvu mpya, hivyo yule mwenye nguvu zaidi hafaidiki na inabidi apoteze baadhi ya nguvu zake kwa sababu kuna mpaka wa kiasi cha nguvu cha kushirikiana.

Hali hii inaonekana kwenye mijadala ya kijinsia, wakati wanaume wanaogopa wanawake kupata nguvu kwa sababu ya athari hasi wanazozikadiria (zitazokuwa) juu ya wanaume. Jamii inaamini kwamba usawa wa kijinsia maana yake wanaume watalazimika kuhamisha baadhi ya madaraka yao na kuwapa wanawake na hivyo wanaume watapoteza nafasi na hadhi zao.

Mtazamo huu juu ya madaraka ambapo upande mmoja unaweza kupata au upande mwengine utakosa, hautaweza kusaidia kufikia jamii pana na isiyo ya kibaguzi.

Ili kufikia malengo yetu, tunatakiwa kubadilisha namna tunavyofikiria wengine katika kutambua madaraka. Hii inamaanisha kutafuta njia ya kuwezesha kazi zetu ziwe zaidi katika namna ya “madaraka ndani ya madaraka” pamoja na ufahamu zaidi wa madaraka kama rasilimali isiyo na kikomo na ipo ya kutosha kwa kila mtu.

Kielelezo nambari 2.6: Walimu Wakuu wanatafakari juu ya Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli

Kupata filamu hii EENET, unaweza kwenda moja kwa moja kwenye vidio kupitia "youtube". Ni onesho la dakika 3 na sekunde 34 linaloonesha walimu wakuu 3 nchini Zambia wakitafakari juu ya majukumu yao ndani ya kamati zao.
https://www.youtube.com/watch?v=EzVJ_hFzP6I&feature =emb_logo

Haya ni maelezo ya filamu

Mwalimu Mkuu - Skuli ya Shungu

Kuelekea upande huu ni kwenda katika kambi ya polisi. Hivyo ni muhimu kwangu kuwaorodhesha kwa sababu ni katika eneo hilo ambapo kuna watu ambao wapo katika Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli; askari polisi, pia tuna watu kutoka kanisani ambao ni wajumbe wa kamati. Aidha, tunao wajumbe wenye ujuzi tafauti kutoka ndani ya jamii, wakiwemo, seremala, fundi mwashi, fundi bomba na wengineo ambao wapo katika kamati za elimu mjumuisho za skuli. Pia tunashirikiana na watu mbalimbali kutoka ndani ya jamii. Watu hao ni muhimu sana kwetu kwani wao wanaweza kuwahudumia Watoto vizuri kuliko tunavyofanya sisi wakati tukiwatembelea majumbani.

Msaidizi Mwalimu Mkuu-skuli ya Sekondari ya Luyaba

Ni vyema kuelewa kwamba, kuanza programu mpya si jambo rahisi. Ni jambo gumu lakini ni lazima ujipe moyo kuhakikisha kwamba programu inafanyika na kusonga mbele.

Jamii tunazozihamasisha na zile ambazo tumezitoa kwenye bodi, wote wanaunga mkono kile kile kilichokuwa kinafanyika katika skuli. Tulilazimika kuunda kamati ambapo watu wenye fani tafauti waliwekwa pamoja ili kubainisha kile tunachopaswa kufanya.

Skuli ya Lubaya ina viongozi 22 kutoka jamii moja, wakati walipohamasika nasi tulihamasika kuunda kamati. Wajumbe wa kamati hizo ni miongoni mwa watu ambao wanasaidia skuli katika utambuzi wa watoto, kuhamasisha matumizi ya rasilimali pale tunapotaka kuendesha programu, au tunapotaka kufanya

kitendo chochote kile.

Kamati ya Elimu Mjumuisho inajumuisha walimu, wajumbe kutoka kada ya afya, na kada ya kilimo na pia, kuna wawakilishi kutoka miongoni mwa viongozi wa vijiji. Ni vyema kubainisha pia, jamii ya wafanyabiashara inahusishwa katika kamati za Elimu mjumuisho. Pia kwenye kamati tunaweza kubainisha maeneo yenye mahitaji na inaweza kutusaidia kuchagua programu mbalimbali. Kamati haina wajumbe wa kudumu ambapo kikawaida inabadilika kwa mujibu wa mahitaji ya skuli.

“Mwanamke anazungumza”

“Na baadaye darasa lilifanyiwa matengenezo, lilikuwa darasa la zamani sana, tulilifanyia matengenezo kupitia Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli. Kwa

kawaida katika kamati tunao wataalamu ambao wanaweza kutusaidia kuwarejesha wanafunzi ambao wapo nje ya skuli na walioacha skuli. Kwa msaada wa watu wa huduma za jamii ambao tunashirikiana nao.”

Kielelezo nambari 2.7: Kuandikisha Wajumbe wa Kamati.

Kitu gani kinamshawishi mtu kujiunga na Kamati ya Elimu Mjumuisho?

Vitu vingi vinaweza kumshawishi mtu kujiunga katika kamati na kila mmoja huwa na sababu zake binafsi za kutaka kujiunga. Tunafikiria kwamba hawakuambiwa na viongozi wao kwamba wajiunge.

Walimu, walimu wakuu au wataalamu wengine wanaweza kushawishika kwa:

- Kujitolea kusaidia wanafunzi wote kuhudhuria, kushiriki na skuli kupata mafanikio katika skuli.
- Kuwa na hamu ya kusoma kutoka kwa wengine na kuimarisha kazi zao na kwa kushirikiana na wanafunzi.
- Kuwa na utayari wa kubadilishana uzoefu na mawazo yao ili kusaidia wenzao ambao bado wanahangaika na uwepo wa elimu mjumuisho.
- Kuwa na hamu ya kuona kazi za Elimu mjumuisho zinapangwa na kuratibiwa kwa ufanisi zaidi.
- Kuweza kuongeza ujuzi mpya au uzoefu kwenye taarifa zao binafsi.

Wanafunzi wanaweza kuhamasika kwa:

- Kuwa na hamu ya kuona sauti zao zinasikika ndani ya skuli juu ya mambo muhimu yatakayowaathiri wenyewe kwa mujibu wa rika zao
- Kuwa na hamu ya kutowa mawazo yao juu ya elimu mjumuisho.
- Kuwa na hamu ya kupata maarifa mapya
- Kuongeza uzoefu ambao siku moja wataweza kutumia kwenye taarifa zao binafsi.
- Kujihisi kuwa ni sehemu ya kupatikana kwa mambo muhimu.

Wazazi, walezi au wahudumu wa watoto pengine watahamasika kwa kujitolea kuwasaidia watoto wao au wanafunzi wengine wanaohitaji msaada katika kujifunza.

- Kujitolea kusaidia watoto wao au wanafunzi wengine kupata msaada wanaouhitaji katika kujifunza
- kuwa na hamu ya kuona sauti zao zinasikika
- Hamu ya kubadilishana uzoefu na mawazo yao ili kusaidia wazee wengine, walezi au wahudumu wa watoto wao kutatua changamoto zinazofanana
- Kuwa na hamu ya kupata maarifa na stadi mpya na kuongeza uzoefu ambao utaingizwa katika taarifa zao binafsi (CV)
- Kuwa na hamu ya kukutana na watu wengine na kuunda urafiki

Ni njia gani zitumike kuwajulisha watu kuhusu kuwepo na kufanya kazi kwa Kamati ya Elimu Mjumuisho ili wahamasike kujiunga?

Kuna njia nyingi za kuwajulisha watu kuwepo kwa kamati. Baadhi zinafaa zaidi kwa kikundi lengwa zikiwemo:

- Mabango katika ubao wa maelezo, yanayoizunguka skuli, chumba cha wafanyakazi nakadhalika
- Barua kutoka kwa mratibu wa kamati au mwalimu mkuu zipelekwe kwa wajumbe wa kikundi lengwa.
- Mkutano wa wazi kuwasilisha kazi ya kamati na kualika wajumbe wapya
- Mkutano au mada katika somo kwa wanafunzi.
- Michezo ya kuigiza au kufanya mambo mengine yanayohusu elimu mjumuisho, kazi ya kamati nakadhalika
- Picha au maonesho ya uchoraji juu ya Elimu Mjumuisho, na ujumbe kuhusu kazi ya kamati na vipi kujiunga
- Kuwepo ujumbe, makala kwenye tovuti ya skuli au kwa vyombo vyengine vya habari kuhusu kamati na watu wengine wenye hamu ya kushiriki katika mkutano ujao.

Kielelezo nambari 2.8: Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli anafanya nini?

Mratibu wa Elimu Mjumuisho anapaswa kufanya kazi ya kuratibu. Hii inamaanisha kupanga na kusimamia, badala ya kuwa na jukumu kamili la utambuzi, upimaji na utoaji wa Elimu Mjumuisho.

Atajitahidi kuongeza uwezo wa kuhakikisha kuwa kunakuwepo tamaduni wa mjumuisho kwa ukamilifu, sera mbali mbali na utekelezaji wa mjumuisho katika skuli.

Kielelezo nambari 2.9: Taarifa za Majadiliano

- Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli lazima awe na ujuzi maalumu kama vile ujuzi wa nukta nundu na lugha ya alama.
- Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli ataweza kufanya upimaji wa utaalamu wa uoni na usikivu
- Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anapaswa kuwa katika kitengo au ofisi ya elimu kwa muda wa saa 8 kila siku ili kuhakikisha kuwa wazazi,walezi au waangalizi, walimu, nakadhalika, wanajua mahala anapopatikana wakihitaji msaada
- Mwalimu ambaye ana uzoefu wa kufundisha wa angalau miaka 20 na sifa za juu anapaswa kuwa na jukumu la kuwa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli
- Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anapaswa kuwashirikisha watoto, wazazi, walezi au waangalizi katika mambo maalumu kila inapowezekana
- Inawezekana mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli kushirikishwa katika kupanga kazi za mtaala wa ziada kama vile michezo na mchezo wa kuigiza
- Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anapaswa kuhudhuruia mikutano ya kamati ya mjumuisho ya skuli kila inapowezekana

Kielelezo nambari 2.10: Sifa za Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli

- **Mstahamilivu** –ana muda wa kusikiliza mapendekezo, matatizo, n.k. atoe fursa ya kuzungumza kwa watu wengine.
- **Anaeingilika** – asiwe na tabia itakayowafanya watu kumuogopa. Wazazi au walezi, waangalizi, walimu, nakadhalika wahisi wanaweza kuleta maswali yao, matatizo yao na kumuomba ushauri.
- **Mwenye stadi nzuri za kusikiliza** – husikiliza mawazo ya wengine. Hazungumzi muda wote na wazazi, walezi au waangalizi, wanafunzi, nakadhalika lakini awe na muda wa kusikiliza na kufahamu mawazo ya watu wengine.
- **Anawajibika**– ana maadili mema ya kazi na anaamini kwamba wanafunzi wote wana uwezo tofauti na wote wanaweza kufikia malengo. Aamini kwamba wanaweza kufanya kazi vizuri kwa uwezo wao wote.
- **Mvumbuzi** – anaweza kufikiria njia mpya na tafauti za kufanya mambo.
- **Mwenye kubadilika** – ana uwezo wa kubadilisha mipango hata wakati wa mwisho; na ana uwezo wa kufikiria njia za kutatua matatizo hata kama kwenye mazingira yenye changamoto.
- **Anajali muda** – hapotezi muda kwa kazi zisizo za lazima. Anapanga namna bora ya kutumia muda ipasavyo.
- **Rafiki na mtaalamu** – ana tabia ya urafiki ambayo inajenga uhusiano mzuri katika kazi.
- **Kigezo kizuri** – awe na tabia bora na mfano kwa wengine, ndani na nje ya mazingira ya kazi. Walimu watachunguza tabia zao kwa wanafunzi, wazazi au walezi, waangalizi na wenzao ili waweze kufuata mfano wao.
- **Anafahamu mbinu pacha katika kujifunza** – ana uwezo wa kuelezea kwamba lazima tulenge katika mabadiliko ya **kiwango cha mfumo** na pia **mahitaji maalumu ya kujifunza** ya kila mwanafunzi. Tunapaswa kuimarisha Elimu Mjumuisho kwa mitazamo miwili; kwa kukuza mabadiliko ya mfumo na kwa kutoa msaada maalumu kwa mahitaji ya ujifunzaji ya mwanafunzi mmoja mmoja.

Kielelezo nambari 2.11: Maonesho ya Igizo-dhima

Nakili kila onyesho katika kadi, ikate vipande na kila kikundi uwape onyesho moja

1. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli amealikwa kuhudhuria mkutano wa kijiji kujadili juu ya idadi kubwa ya wanafunzi walio nje ya skuli. Mkutano umepangwa na kuongozwa na mkuu wa kijiji ambaye hajui nini cha kufanya juu ya wanafunzi hawa. Waliohudhuria mkutano ni pamoja na kikundi cha wanawake wa kijiji, mwalimu mkuu kutoka skuli inayohusika, baadhi ya wazazi, wazee wa kijiji na wanajamii. Mratibu wa Elimu Mjumuisho katika skuli alichelewa kufika, alipofika hakuzingatia kilichokuwa kinazungumzwa kwani alikuwa anazungumza na simu wakati wa mkutano. Hakuchukua dondoo za mkutano. Hakuzungumza na mtu yeyote wala hakupanga kukutana na wanafunzi.

2. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli huchunguza somo ili kupima njia za kufundishia za mjumuisho. Hufika kabla ya somo kuanza na kumtaka mwalimu amuoneshe andalio la somo. Kisha yeye hukaa nyuma ya darasa huku akiwa kimya wakati wa somo linaendelea na kuchukua nukta za maelezo Baada ya somo huzungumza kwa utulivu na mwalimu mmoja mmoja huku akionesha mambo mazuri ambayo mwalimu aliyafanya katika ufundishaji wake wa somo kabla ya kubainisha maeneo ambayo mwalimu anapaswa kuyafanyia mabadiliko katika ufundishaji wake ili kuufanya mjumuisho kuwa mjumuisho zaidi.

3. Bibi hufika kwenye kitengo ambacho sasa kinaitwa kituo saidizi cha ujifunzaji. Anafadhaika na kulia kwa sababu wajukuu zake wawili 'watukutu' wanaendelea kutoroka skuli na kujiingiza katika matatizo. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anakaa kimya na hana wakati wa kuzungumza naye. Mratibu wa Elimu Mjumuisho hana urafiki na anapozungumza ana tabia ya kuzungumza kwa hasira wala hampeleki bibi kwa mtu mwengine yeyote ambaye angekuwa na muda wa kumpa msaada na ushauri.

4. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli amealikwa kwenye mkutano wa kuimarisha skuli ambapo walimu wanatoa malalamiko yao kwamb wanafunzi ni wengi darasani na walimu hawana muda wa kutekeleza mjumuisho ipasavyo. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anawasikiliza kwa utulivu shida zao na kupanga muda mwengine wa ziada ili kuja skuli kukagua na kuchunguza masomo pamoja na kutoa ushauri kwa walimu. Anawahakikishia kuwa kufuatia ukaguzi na uchunguzi wake watakaa pamoja na kupata suluhisho la changamoto zao; hii ina maana kwamba anaweza kuanzisha mafunzo ya ziada juu ya mikakati ya kufanikisha darasa la elimu mjumuisho.

5. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli, pamoja na mwalimu mkuu, hutembelea nyumba ya wazazi wa mtoto mwenye ulemavu wa akili. Mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 9 na hajawahi kwenda skuli. Wazazi wanamlinda kupita kiasi na hawataki aonewe. Hata hivyo, pia wanafikiri kuwa hahitaji kwenda skuli au kupatiwa elimu kwa sababu 'hataweza kufanya chochote'. Mwalimu mkuu na Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli wanawaelezea ni kwanini mtoto anapaswa kuhudhuria skuli na wanafanya bidii ili kuwafanya wazazi wahisi ni rahisi kumpeleka skuli na kusoma. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anaelezea kwa upole jinsi skuli itakavyofanya bidii kuhakikisha mtoto haonewi na anajumuishwa.

6. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli amealikwa kuzungumza kwenye mkutano wa Uongozi wa Elimu wa Wilaya. Jukumu lake ni kutoa mwamko juu ya hali iliyopo katika skuli za mitaa au vijiji na kutoa maelezo ya kina kuhusu Idara nyengine za wizara, mashirika yasio ya kiserikali (NGOs), nakadhalika, ambao ni sehemu ya mtandao unaofanya kazi zaidi katika skuli za mjumuisho. Wakaguzi wa skuli hawafahamu kikamilifu ElimuMjumuisho na wanaendelea kuuliza maswali juu ya wanafunzi wenye ulemavu na skuli maalumu. Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli hatoi ufafanuzi wa wazi au kupendekeza kuzitembelea baadhi ya skuli pamoja na wakaguzi. Haonekani kuwa na mpango ambao utasaidia kuhamasisha wakaguzi na wafanyakazi wenzake.

Kielelezo nambari 2.12: Muonekano wa Mtazamo wa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli

Kielelezo nambari 2.13: Mifano ya Vitendo ambavyo Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli anaweza Kushiriki

Katika skuli

- Kujenga uwezo na kuhamasisha usimamizi wa skuli, kwa walimu na wafanyakazi wengine wa skuli ambao si walimu
- Kuhakikisha mipango ya skuli ni ya mjumuisho zaidi
- Kutathmini mazingira ili yaweze kufikika
- Kutoa ushauri katika kutengeneza rasilimali mahsusi.
- Kutoa mafunzo ya kimkakati katika madarasa ya Elimu mjumuisho.
- Kukuza ushirikiano kati ya skuli na jamii.
- Kumchunguza na kumpima mwanafunzi mmoja mmoja.
- Kuandaa majadiliano ya vikundi kwa walimu na wanafunzi.
- Kupendekeza vitendo kwa ajili ya dhana ya mjumuisho kwa skuli nzima.

Katika jamii

- Kukuza uelewa katika ngazi ya jamii.
- Kujenga ushirikiano kati ya skuli na jamii.
- Kutembelea wanapoishi wanafunzi maalumu inapobidi.
- Kuhudhuria mikutano inayofanyika kwenye jamii.
- Kufanya rufaa kwa huduma zinazopatikana kwenye jamii. Kwa mfano, kufanya uchunguzi wa kitabibu hospitalini.
- Kubainisha maarifa na vifaa vya kujifunzia na kufundishia ambavyo vinapaswa kutumika katika skuli.
- Kutoa mafunzo kwa watu wanaojitolea ili kuwatambua watoto walio nje ya skuli.
- Kuandaa mafunzo ya kitaalamu kwa wazazi, walezi na waangalizi pale inapohitajika.

Wizara ya Elimu - ngazi ya sera

- Kuhudhuria mikutano ya serikali za mitaa ili kukuza mwamko na uelewa juu ya fedha zilizopo.
- Kutoa mwamko kwa vyombo vya habari - redio na magazeti ya ndani.
- Kuandaa mikutano ya upangaji ili kuhakikisha kuwa mipango yote ni ya mjumuisho.
- Kushirikisha taasisi zisizo za kiserikali (NGOs) na mashirika ya kijamii katika kila mafunzo yanayohusiana na Elimu Mjumuisho kama njia ya kusaidia elimu hiyo au kutoka vyanzo vyengine vinavyofaa.

Kielelezo nambari 2.14: Hadithi ya Jabir

Jabir ana umri wa miaka 12 na anaishi na bibi yake ambaye ni mzee na mwenye ulemavu. Wazazi wake wamefariki. Mara nyingi hahudhurii skuli au huchelewa kufika. Yeye hufanya kazi kwa bidii anapokuwa skuli ingawa wakati mwengine anaonekana amechoka sana. Kamwe hamalizi kazi ya nyumbani na mwalimu wake anafikiria kuwa ataachwa nyuma ikiwa ataendelea hivi. Mara nyingi anaonekana mchafu na asiyejali.

Mpango wa kumsaidia Jabir
Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli atafanya yafuatayo:

- Kuhudhuria mkutano wa skuli kujadili hali ya Jabir.
- Kumchagua mtu kutoka skuli ambaye atatembelea jamii na nyumbani kwao Jabir ili kukusanya taarifa zake. Skuli inapaswa kujitahidi kujua sababu ya hali yake mbaya.
- Kutenga muda wa kuzungumza na Jabir pamoja na bibi yake ili kujua hali ya maisha yake ya skuli na nyumbani.
- Kuanzisha mpango wa kuiwezesha jamii kumsaidia Jabir aweze kumtunza bibi yake na yeye mwenyewe.
- Kuanzisha mpango wa kuisaidia skuli kwa msaadarika kumsaidia Jabir ili kufanikisha kazi yake ya nyumbani.
- Kuhakikisha wafanyakazi wote wa skuli wanaijali hali ya Jabir.
- Kufuatilia hali ya nyumbani kwao Jabir inavyoendelea wakati zinapofanyika ziara za kumtembelea mara kwa mara.

Kielelezo nambari 2.15: Kufanya kazi kuelekea Mjumuisho

Kisa mafunzo cha 1: Darasa lisilofikika

Kisa mafunzo cha 2: Choo cha Wasichana

Kisa mafunzo cha 3: Masomo ya Sayansi ya Bwana Mohammed

Bwana Mohammed anafundisha somo la sayansi katika ngazi ya skuli ya msingi. Ana wanafunzi watatu wenye mahitaji maalumu katika darasa lake lakini hawafundishi. Hukaa nao darasani lakini hawajali kabisa. Alipoulizwa juu ya hili alisema hana ujuzi na nyenzo za kuwafundisha. Wanafunzi ni:

- Khamis - jicho moja halioni kabisa na huona kwa asilimia hamsini (50%) katika jicho lililobaki.
- Fatma - mkimya sana na ana aibu. Anajitenga peke yake na anakuwa hajibu maswali.
- Laila – hawezi kuzungumza vizuri na kuwasiliana. Anaweza kutoa sauti lakini maneno yake hayafahamiki vizuri.

Kisa mafunzo cha 4: Hadithi ya Fatma

Fatma ana umri wa miaka 16. Ana ulemavu wa viungo na anatumia kiti cha magurudumu mawili. Siku zote, Fatma na marafiki zake huhudhuria skuli ya msingi ya kijijini kwao na kufaulu kwa kupata alama za juu. Sasa amesimamishwa na kuendelea na masomo ya ngazi ya sekondari kwa sababu skuli haifikiki kwa kutumia viti vya magurudumu mawili. Sasa hivi anabakia nyumbani siku nzima bila ya kufanya chochote.

Kisa mafunzo cha 5: Skuli ya Zanzibar

Mshauri wa nje kutoka Wizara ya Elimu aliitathmini skuli ambayo ilikuwa katika eneo la kijijini. Mshauri alijuilishwa kuwa skuli hiyo ilikuwa ni ya mjumuisho kwa sababu 'ina watoto wengi wenye ulemavu'. Moja ya matokeo kutoka kwenye tathmini aliyoifanya ni kwamba skuli na madarasa hayakuwekewa vifaa vyovyote vya kujifunzia. Kuta kwenye madarasa na koridoo zilikuwa tupu bila ya machapisho na vifaa vinavyohitajika. Watoto wengi wanaosoma katika skuli hiyo wana ulemavu wa usikivu. Mshauri alipouliza ni "kwanini hakukuwa na vifaa vya kujifunzia au machapisho ya kazi za wanafunzi kwenye kuta". Jibu lilikuwa kwamba, "walimu hawana madarasa yao wenyewe hivyo hulazimika kuhama kutoka darasa moja hadi jengine kwa kila somo."

Kisa mafunzo cha 6: Malalamiko ya jamii kuhusu uonevu

Wazazi na wanajamii wametoa taarifa skuli kwamba idadi kubwa ya wanafunzi wanashambuliwa, kupigwa na kuonewa wanapokwenda skuli. Wahalifu ni kikundi cha wanaume wakubwa ambao wameacha masomo.

Wanawashambulia, wanawaonea na kuwaibia chakula na fedha wakiwa njiani kuelekea skuli. Baadhi ya wanafunzi hawa sasa wanaogopa kabisa kwenda skuli na badala yake hubakia nyumbani au huzunguka mitaani siku zote. Kiongozi wajamii na baadhi ya wazazi kadhaa wanakuja skuli kuomba msaada wa kutatua tatizo hili.

Kielelezo nambari 2.16: Wanafunzi, Wazazi na Walezi wanasema nini?

Wanafunzi, wazazi na walezi wanatoa ushauri chanya juu ya namna ambavyo skuli zao zitaimarika na kutoa huduma zilizo bora. Uimarishaji walioupendekeza ni kama ifuatavyo:

- Kuwataka wanafunzi kubainisha wale wanayohitaji.
- Kuitisha mkutano kuelezea masuala mbalimbali ya kitaaluma kwa wazazi na walezi.
- Kuwashauri wazazi au walezi kuainisha mahitaji, kujifunza namna ya kuwajali watoto wao na kuweka mikakati ya utatuzi wa matatizo kwa changamoto zinazowakabili.
- Kuwashirikisha wazazi au walezi katika kutoa ushauri nasaha.
- Kuifanya skuli kuwa ni sehemu rafiki kwa wote.
- Kuondosha uonevu na unyanyasaji na kuwafanya wanafunzi wote kuwa sawa bila ya kujali dini zao, matabaka yao au kuwa na mahitaji au kutokuwa na maalumu.
- Kutoa mafunzo kwa walimu ili kuwa na uwezo wa kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji ya ziada ya kielimu.
- Kuwaongezea posho walimu wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- Kuimarisha ushirikiano baina ya walimu, wanafunzi na wazazi wao.
- Kutafuta njia za kuwafundisha wanafunzi ili kuwa wazungumzaji wazuri na sio kuzungumza kwa ujeuri.
- Kuwafanya wanafunzi wote kuwa na usawa.
- Kuwasomesha wanafunzi wote kwa usawa bila ya kuwabagua
- Kuwapatia zana maalum (vifaa saidizi).
- Kuwashirikisha kwenye michezo pamoja na kuwapatia vifaa.
- Kuandikisha wanafunzi zaidi, wenye mahitaji maalum ya kielimu na wenye ulemavu.
- Kutoa mwamko kuhusiana na Elimu Mjumuisho katika skuli na kwenye jamii.

- Kuielimisha jamii umuhimu wa kuwapeleka skuli watoto wenye aina zote za ulemavu.
- Kuwashirikisha wazazi au walezi katika shughuli za mtaala, hususan mtaala wa ziada.
- Kuwapa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada ya kielimu majukumu ya kiuongozi.
- Kufanya kazi na taasisi hisani, kuwapatia nyenzo zitakazowawezesha wanafunzi wenye ulemavu kufika skuli na kuzipunguzia ada familia za wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- Kujenga madarasa mengi
- Kuhakikisha kwamba wanafunzi na walimu wanakuwa na tabia njema.
- Kuwapatia maji safi na salama kwa ajili ya kunywa na shughuli za usafi ndani ya skuli
- Kufanya mazingira ya skuli kuwa safi na yenye miti ya kutosha.
- Kuhakikisha kwamba walimu na wazazi wanafanya kwa ushirikiano
- Kuhakikisha kunakua na huduma bora kwa ajili ya wanawake zikiwemo vyoo na vyumba vya faragha
- Kuwa na viwanja bora vya michezo, pamoja na shughuli nyengine za burudani
- Kuwapatia zana bora za kujifunzia
- Kuwasaidia kwa kuwalipia ada wanafunzi ambao ni masikini zaidi
- Kuwapatia elimu bila ya malipo wanafunzi wenye ulemavu
- Kuwapa mafunzo walimu kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu au wenye ulemavu.
- Kuwa na programu maalumu za chakula ndani ya skuli.
- Kuwapatia usafiri wanafunzi wenye ulemavu na wale wote wanaoishi mbali na skuli.
- Kuwapatia huduma za dahalia wanafunzi wote wanaohitajia.

Kielelezo nambari 2.17: Igizo dhima la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli

Nakili kila igizo katika kadi, ikate vipande na kila kikundi uwape igizo moja.

1. ‘Siku ya wazazi’ ya mjumuisho - jamii na skuli

Siku hii ya wazi' imepangwa kuwaalika skuli wazazi, walezi, waangalizi na wanajamii. Inapaswa kuwa ni siku ya kupeana taarifa, mambo ya kufurahisha, na kuonesha kazi za wanafunzi na maendeleo yao. Imepangwa kuwa ni siku ya kujenga ushirikiano kati ya skuli na jamii na kukuza mwamko juu ya mjumuisho. Igizo dhima lako liwe kuhusu kikao cha kupanga mkutano ambapo labda mwalimu mkuu au mjumbe wa Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli atasimamia mkutano na Mratibu wa Elimu Mjumuisho katika skuli akiwa kama mshauri.

2. Programu za ushauri na usaidizirika – kazi ya kamati miongoni mwa walimu

Programu ya ushauri na usaidizirika miongoni mwa walimu katika skuli yoyote ile inamaanisha kuwa njia za kufundishia zitakuwa anuwai na bora, na walimu watakuwa mjumuisho zaidi wanapochunguza na kusaidiana baina yao na kubadilishana mawazo na ujuzi.

Igizo dhima lako litakuwa ni sehemu ya mrejesho baina ya walimu na mratibu wa elimu mjumuisho katika skuli. Inapaswa kuweka wazi ni nini haswa kinachotokea skuli kama sehemu ya ushauri na msaada kwa wafanyakazi wa rika moja wa skuli. Inapaswa kujibu maswali yafuatayo:

- Ni jinsi gani walimu wanasaidiana baina yao na kubadlishana maarifa?
- Ni kwa namna gani walimu wanashirikiana katika kutumia nyenzo?
- Ni kwa nini ushauri na msaada wa rika ni muhimu kwa maendeleo ya kitaalamu ya walimu na mjumuisho bora wa wanafunzi?
- Ni vitendo vipi vinafanya sehemu ya programu?
- Mafunzo na msaada gani unatolewa kwa walimu wapya wanaofika skuli?
- Ni nani anayefaidika kupitia utekelezaji wa programu?
- Ni kwa vipi kila mfanyakazi anaweza kuhusishwa?

3. Kuyafikia mazingira yaliyozunguka – jamii na skuli

Walimu wanapaswa kuhamasishwa kutathmini mazingira ya jamii iliyowazunguka na kufikiria jinsi watakavyoimarisha. Kwa mfano, je mwanafunzi ambaye ana matatizo ya kutembea kwa miguu au anayetumia kiti cha magurudumu mawili (kiti mwendo) angeweza kwenda skuli?

Mwanafunzi angeweza kutembea katika jamii kwa usalama na kwa kujitegemea? Walimu na wanajamii, kwa mfano, Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli inapaswa kuitembelea jamii na kutafakari juu ya maeneo ambayo wanafunzi wanapita na kutembea wanapokuwa wanakwenda na kurudi skuli. Wangeweza hata kuvipiga picha vizuizi vyovyote vinavyowakabili wanafunzi na kupendekeza njia za kuvitatua vizuizi hivyo. Hii inaweza kusababisha kuongeza ufahamu katika jamii na pia kujadiliwa wakati wa ‘Siku ya Wazazi’.

Igizo dhima lako linapaswa kuonesha hatua anazozichukua mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli katika kuanzisha kufanyika kwa tathmini ya mazingira ya jamii.

4. Kuwasaidia wanafunzi walio katika kipindi cha mpito.

Katika kipindi cha mpito kutoka skuli moja kwenda nyingine ni wakati muhimu kwa mwanafunzi yeyote na mara nyingi ni wakati ambapo wanafunzi huacha skuli hususan kwa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada (wenye mahitaji maalum ya kielimu au wenye ulemavu). Maandalizi na kupanga katika kipindi cha mpito ni muhimu sana.

Igizodhima lako linapaswa kulenga maandalizi ya mkutano kuhusu kipindi cha mpito la kijana wa kiume ambaye ana shida ya kutembea. Anaweza kutembea polepole kwa kutumia magongo lakini hali yake mara nyengine humchosha kwa hivyo mara nyengine hutumia kiti cha magurudumu mawili (kiti mwendo).

Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli anapaswa kuongoza mkutano. Wanaohudhuria mkutano wanapaswa kuwa mtoto wa kiume, wazazi wake, marafiki, na walimu wakuu kutoka skuli mbili. Unaweza kuamua ni nani mwengine muhimu ili awe ni sehemu ya mkutano.

Mapendekezo ya kuongoza igizo dhima lako ni kama yafuatayo:

- Tarehe ya mkutano ni lini mchakato wa kupanga unapaswa kuanza?
- Umbali na hali ya barabara kutoka nyumbani hadi skuli mpya
- Mazingira ya kimaumbile ya skuli mpya
- Msaada rika
- Kinachopaswa kufanywa kabla ya kwenda skuli mpya
- Kinachopaswa kufanywa baada ya kuanza skuli mpya
- Mafunzo yanayohitajika katika skuli mpya na kwa ajili ya nani

Hiyo hapo juu ni orodha ya mapendekezo yanayopaswa kuongoza igizo dhima lako. Kikundi chako kinaweza kutoa mawazo ya ziada. Unapaswa kuonesha kwa uwazi jukumu la mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli katika kuwezesha mabadiliko bila ya tatizo au vikwazo.

5. Kutumia ujuzi na rasilimali zilizopo

Skuli nyingi hususan za vijijini, mara nyingi zina rasilimali chache na fedha kidogo za kununulia vifaa vipya. Hii inaweza pia kuwa ni changamoto katika kutunza na kubadilisha vifaa vya skuli na majengo kutokana na vizuizi vya bajeti. Changamoto nyingi zinaweza kuepukwa kwa kuihusisha jamii na kubaini ujuzi na rasilimali (pamoja na rasilimali watu) ambazo zinapatikana katika jamii.

Igizo dhima lako linapaswa kuwa ni mkutano wa kijiji ambao mratibu wa Elimu mjumuisho wa skuli atabaini msaada ambao unaweza kupatikana. Mapendekezo ya kuongoza igizo lako ni kama ifuatavyo:

- Vifaa vya darasani vinahitajika kwa somo la hisabati na sayansi. Ni nani anayeweza kutengeneza hivi?
- Wanawake ambao wanaweza kufundisha kushona
- Msada wa darasa kwa watoto wenye mahitaji ya kibinafsi
- Kuanzisha bustani ya skuli
- Kusafisha uwanja wa skuli kwa matembezi rahisi
- Kuanzisha kikundi cha kusoma katika jamii
- Kutengeneza njia kwenye madarasa ambayo wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanaweza kupita kwenye madarasa
- Wanaosaidia kufanyika kwa shughuli za michezo.

Hapo juu ni orodha ya mapendekezo ya kuongoza igizo lako. Hulazimiki kufuata haya kama yalivyo badala yake unaweza kutumia mawazo mengine kutoka kwenye kikundi chako. Tafadhali onesha wazi jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli katika mchakato huu wote.

Kielelezo nambari 2.18: Matumizi Bora ya Vituo Saidizi vya Ujifunzaji

Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli, walimu na wafanyakazi wanaweza kutumia vituo wezeshi vya ujifunzaji. Kwa ajili ya:

- Kutengeneza na kutumia rasilimali, kwa mfano, michoro mikubwa ya kuchapa na kugusa, vifaa maalumu vya somo la hisabati, picha, kadi za maneno, nakadhalika
- Kutathmini mahitaji ya mwanafunzi mmoja mmoja
- Kuandaa andalio la somo, kutengeneza karatasi lengwa na mipango ya Elimu Mjumuisho, nakadhalika
- Kuandaa mpango binafsi wa elimu kwa masomo ya msaada ya mtu mmoja mmoja kuunga mkono ujifunzaji wa darasani
- Kutoa mafunzo ya ualimu kwa ajili ya kukuza Elimu Mjumuisho
- Kuandaa mikutano na wazazi au walezi.

Rejea

LEWIS, Ingrid (2012). Kikundi lengwa. Enabling Education Review: Mecedonia. www.eenet.org.uk/enabling-education-review/enabling-education-review-1/eer-1/1-2/

LEWIS, I (2005). Making a difference: Training materials to promote diversity and tackle discrimination, Save the Children.

EENET (2020). Utafiti …… Kusini Mashariki mwa Afrika